Ijumaa Februari 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581581

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



**SERIKALI YA HONG KONG SASA YAWAJIA JUU MESSI, MIAMI**

UKURASA 22

**CHADEMA** yaita CCM kushiriki maandamano



UKURASA 2

**Watembelea** The Guardian kujifunza uzalishaji maudhui

UK.4

**Utoaji** wa mimba wachangia 10% vifo vitokanavyo na uzazi nchini

UKURASA 4

# Samia: Mabalozi msiingilie uchaguzi



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, katika sherehe za mwaka mpya kwa mabalozi hao, Ikulu jijini Dar es Salaam juzi usiku. **PICHA: IKULU**

• **ASISITIZA** utakuwa huru na wa haki... *Endelea Ukurasa 2*



UKURASA 2

# Vilio vyatawala dola kuadimika

# Bunge lashtukia 'kulikoni' akaunti mpya ya Escrow

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, AZAM MECHI YA KIBABE UK.24

**MAONI** UK.6

# Vilio vyatawala dola kuadimika

**Na Restuta James**

BAADHI ya wafanyabiashara Dar es Salaam wamelalamikia uhaba wa Dola ya Marekeni katika mzunguko wa fedha hatua ambayo imesababisha kuibuka kwa upatikanaji wa njia ya magendo, Nipashe imebaini.

Wakati hali ikiwa hivyo Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imesema tatizo hilo ni himilivu kutokana na kuwapo kwa akiba ya kutosha. BoT imebainisha kwamba kuna akiba ya Dola za Marekani bilioni 5.3 ambazo zinazotosha kufanya miamala ya ununuzi wa bidhaa kwa kipindi cha miezi mitano kuanzia sasa.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wafanyabiashara walisema hali ya upatikanaji wa sarafu hiyo ambayo hutumika katika uagizaji wa bidhaa kutoka nje imezidi kuwa mbaya na kwamba wakienda kununua benki hawapati.

Sebastian Michael, anayeuza nguo katika soko la Kariakoo alisema: "Hata zile tulizokuwa tunanunua kimagumashi (kiyemela) sasa hivi hazipatikani. Hali imezidi kuwa mbaya."

Alisema mwezi uliopita, walikuwa wananunua Dola moja hadi Sh. 2,700 kwa wafanyabiashara wenzao, ambao nao wanaziuza kwa uchache ili wabakie na akiba kwa matumizi binafsi.

"Kwa sisi wafanyabiashara wadogo tunaohitaji kwa ajili ya kulipia kutoa mizigo kwa mawakala wa usafirishaji, tukienda benki hatupati kabisa. Wanauzia watu wao (wafanyabiashara wakubwa). Kwa sasa sina kabisa nguvu ya kutafuta dola. Kuna dada yangu yeye anafanikiwa kuuziwa na benki kwa hiyo nikibanwa sana namtafuta ananisaidia," alisema.

Mmoja wa wafanyakazi katika hoteli ya kitalii Dar es Salaam, ambaye hakutaka jina litajwe, alisema hawapeleki dola benki kwa kuwa nao wanaziuza kwa wahitaji.

Kutokana na kuadimika kwa Dola, imebainika kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanatumia fursa hiyo kuwauzia wenzao kwa bei ya juu tofauti na bei elekezi.

"Unakuta mfanyabiashara anahitaji Dola 20,000 akalipie mzigo kwa wakala. Benki hawatoi zaidi ya Dola 2,000 kwa kila mteja kwa siku, hivyo ili uipate yote hiyo itakulazimu uzunguke zaidi ya benki 10 au uende benki hiyo moja siku 10. Lakini kuna mwenzako anazo sema ana kiwango chake," alisema mmoja wa wafanyabiashara hao (jina linahifadhiwa).

Pamoja na Dola kuuzwa kwa bei ya juu katika masoko yasiyo rasmi, bei elekezi inataka maduka yenye leseni na benki kuuza Dola moja kwa Sh. 2,525.

Mfanyabiashara na kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Godbless Lema, alisema hakuna Dola mtaani na kwamba ulanguzi wa sarafu hiyo unazidi kuota mizizi.

"Hakuna kabisa Dola, kuagiza bidhaa imekuwa ngumu. Mkifanya mzaha umaskini unaenda kuchafua hii nchi. Huku mitaani wananchi wanapiga yowe, hali ni mbaya," alisema na kuongeza kuwa kampuni kubwa zinatafuta dola kwa pikipiki mtaani na ziko tayari kununua kwa bei kubwa.

**KAULI YA BoT**

Mkurugenzi wa Utafiti na Sera wa BOT, Dk. Suleiman Missango, alikiri kuwa kuna upungufu wa fedha za kigeni lakini hali bado ni himilivu.

"Hali haijatengemaa kwa hiyo majibu yetu ni kama ya mwaka jana kwamba akiba tuliyo nayo inatutosha kulinganisha na majirani zetu. Hakuna sababu ya wananchi kupaniki. Safari hii hatujanunua Dola sokoni kwa hiyo ile iliyoingia kupitia utalii na mauzo ya nje ya mazao tumeiacha kwenye mzunguko," alisema.

Alisema Novemba hadi Desemba, mwaka jana, nchi ilipata Dola za Marekani kutokana na msimu wa utalii ulioiingizia nchi fedha za kigeni pamoja na uuzaji wa mazao ya biashara nje ya nchi.

Pia alisema korosho, pamba na tumbaku, ziliingizia nchi fedha za kigeni ambazo serikali iliamua zibaki kwenye mzunguko badala ya kupelekwa BoT.

"BoT tunaona hali ya fedha za kigeni haijabadilika sana tangu tulivyoongea. Hizi changamoto zinatokana na sababu za nje ya nchi zaidi. Hatuna haja ya kupaniki, hatuko kwenye hali mbaya," alisisitiza.

Dk. Missango alisema taarifa zilizopo mitaani ndizo zinasababisha taharuki na uhaba wa dola kinyume cha hali halisi, jambo linalofanya bei ya dola ipande.

Mwaka jana, alisema Benki Kuu za nchi zenye uchumi mkubwa duniani zilipunguza ukwasi katika uchumi huku Marekani ambayo ndiyo inachapisha Dola ikiongeza riba kutoka asilimia 0.75 hadi asilimia 5.2, ambalo ni ongezeko la asilimia 500.

Alisema katika kipindi cha miezi mitatu ijayo, upatikanaji wa dola utaimarika zaidi kwa kuwa nchi itaingia kwenye msimu wa utalii.

Dk. Missango alisema taarifa ya maoteo ya mwenendo wa uchumi wa dunia iliyotolewa na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha Duniani (IMF) na mashirika mengine ya kimataifa inaonesha kwamba bei za mafuta na bidhaa zingine zitashuka.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge kwenye kipindi cha maswali ya hapo kwa papo, Bungeni Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia: Mabalozi msiingilie uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewahakikishia mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa kwamba serikali itahakikisha uchaguzi unafanyika kwa misingi ya uhuru na haki.

Sambamba na hayo, Rais Samia amewaonya mabalozi kuhusu kuingilia uchaguzi huo kwa kuzingatia mila, kanuni na maadili ya kidiplomasia.

Tanzania inatarajia kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa (viongozi wa mitaa, vijiji na vitongoji) baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwakani.

Rais Samia alisema hayo juzi jioni wakati akizungumza na mabalozi na wawakilishi wao Ikulu, Dar es Salaam, kwenye sherehe za Mwaka Mpya wa Kidiplomasia.

Pia alisema serikali itahakikisha amani na utulivu vinatawala katika kipindi chote cha uchaguzi kwa gharama yoyote na kuhakikisha sheria na utawala bora vinadumishwa kwa watu wote katika kipindi chote cha uchaguzi.

Kuhusu miswada mitatu ya sheria iliyopitishwa hivi karibuni na Bunge, alisema ataitia saini na kuwa sheria. Miswada hiyo ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 2023.

Rais Samia alisema anaamini kwamba kupitishwa kwa miswada hiyo na kutiwa saini kuwa sheria kamili, kutasaidia uchaguzi kufanyika kwa uwazi, uhuru na haki. "Tumepeleka miswada mitatu bungeni ambayo Februari 2, mwaka huu, Bunge liliipitisha na mimi nitaisaini (nitatia Saini) ili iwe sheria na kupitia hiyo, tutahakikisha uchaguzi unakuwa wazi, huru, haki na amani na utulivu inaimarishwa katika kipindi chote cha uchaguzi na kwa gharama yoyote," alisema Rais Samia.

Alisema katika kuhakikisha uchaguzi nchini unakuwa huru na wa haki, Kikosi Kazi cha Kupitia na Kushauri Mageuzi muhimu katika mfumo wa siasa kiliundwa na kuwasilisha ripoti yake mwaka jana.

Kwa mujibu wa Rais, mapendekezo mengi ya kikosi kazi yaliyopokewa na serikali na wadau wote, yalihusu kuongeza uwazi katika michakato ya uchaguzi ikiwa ni pamoja na uteuzi wa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Rais Samia alisema ni masuala machache tu ambayo hayakupokewa moja kwa moja ambayo yalikuwa kinyume cha Katiba na kwamba mambo hayo yanaweza kuchukuliwa wakati wa mchakato wa marekebisho ya katiba.

Aidha, Rais alisema serikali itaendeleza ushirikiano wa kidiplomasia na nchi mbalimbali kwa mujibu wa katiba, tunu za kitaifa, usawa, umoja na mshikamano wa kitaifa.

Hata hivyo, alieleza kusikitishwa kwake na mapigano yanayoendelea Ukanda wa Gaza ambayo yamesababisha mauaji ya watoto na raia wasio na hatia. Aliunga mkono usuluhishi kati ya Palestina na Israel huku akitoa wito wa kusitishwa mapigano na kupatiwa misaada ya kibinadamu.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema msisitizo wa Tanzania kwa washirika wa kidiplomasia ni kuendelea kuzingatia, kuheshimu taratibu na miiko ikiwamo kuheshimu mila na utamaduni wa kidiplomasia wa kila nchi.

Makamba alisema Tanzania itaendelea kutoa na kuimarisha ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha washirika wake wote wa kidiplomasia wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

# CHADEMA yawaita CCM kushiriki maandamano

**Na Vitus Audax,** MWANZA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimewaita wananchi, wakiwamo wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanaokerwa na ugumu wa maisha, kushiriki katika mwendelezo wa maandamano yake yanayotarajiwa kufanyika Februari 15, mwaka huu jijini Mwanza.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Tanzania Bara, Benson Kigaila, alitoa rai hiyo wakati akitangaza kusogezwa mbele kwa maandamano hayo yaliyotarajiwa kufanyika Februari 13, mwaka huu kutokana na uwanja kuwa na matumizi mengine.

Kigaila alisema maandamano hayo ya awamu ya pili yatafanyika katika barabara za Jiji la Mwanza na kuhitimishwa kwenye Viwanja vya Furahisha kwa mkutano na wananchi utakaohudhuriwa na viongozi wote wa CHADEMA kitaifa.

"Maandamano ya Mwanza si ya CHADEMA tu, bali ni ya watanzania wote wanaokerwa na ugumu wa maisha. Hivyo, tunawaita wana CCM waje tushirikiane kuidai serikali kuja na mpango madhubuti wa kudhibiti ugumu huu kwani kwa sasa wote tunaisoma namba," alisema Kigaila.

Alisema wanaendelea vizuri na maandalizi na taarifa ya maandamano tayari imepelekwa kwa wakuu wa polisi ngazi za wilaya yatakakofanyika maandamano hayo kwa mujibu wa sheria.

"Tayari tumewajuza polisi siku saba kabla ya maandamano licha ya sheria kututaka kuwasilisha taarifa ndani ya siku mbili, hivyo tumewaahidi zaidi na tunatarajia kuwa na njia tatu za maandamano ambazo zitaungana katika eneo la Bustani ya Grand-Hall kisha kuelekea katika Viwanya vya Furahisha," alisema Kigaila.

## HABARI KITAIFA

# Bunge lashtuka uanzishaji akaunti mpya ya Escrow

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limezuia uanzishwaji akaunti maalum ya Escrow, ambayo ilikuwa ianzishwe kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi na kutangaza utalii.

Vilevile, limeazimia serikali ianzishe Mfuko wa Maendeleo ya Utalii (TDL), ambao utachangiwa na asilimia moja ya mauzo yote ya nje yanayoingia nchini kutokana na shughuli za utalii.

Malengo ya kuanzishwa akaunti hiyo ni kutoa asilimia sita, yaani asilimia tatu kwa ajili ya uhifadhi na asilimia tatu kwa ajili ya kutangaza utalii kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

Fedha hizo zingewekwa katika akaunti hiyo na taasisi hizo zingetakiwa kuorodhesha mahitaji yake na kuyapeleka hazina kwa ajili ya matumizi ya fedha hizo.

Jana wakati anawasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2023, Mwenyekiti wake, Timotheo Mnzava, alisema uchambuzi wake umebaini uanzishwaji akaunti hiyo unatoa mwanya fedha za umma kuchezewa kwa kuwa wazo lake halitokani na mpango wa bajeti, sheria yoyote ile wala ushauri wa Bunge.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki

Alisema utaratibu wa kufungua akaunti maalum hufanyika pale panapokuwa na mgogoro wa pande mbili juu ya mgawanyo wa mapato ya fedha zao, hivyo pande hizo hutunza fedha hizo katika akaunti hiyo hadi pale suluhu ya mgogoro itakapopatikana.

Mwenyekiti huyo alikwenda mbali zaidi, akasema kuna swali la kujiuliza kama kuna mgogoro wa mgawanyo wa mapato kati ya taasisi hizo na Hazina.

"Fedha zinazokuwa kwenye akaunti hii maalum, hata ukaguzi wa matumizi yake, huwa si wa kawaida.

"Kamati inaona suluhu pekee ya kushughulika na matatizo ya taasisi hizi za uhifadhi, ni kuhakikisha wanabaki na sehemu ya fedha wanazokusanya kwa ajili ya taasisi hizi kujiendesha kwa ufanisi kwa kuzingatia aina na mazingira ya kazi zao.

"Hii itahakikisha kuwa matumizi ya fedha hizi ambazo ni fedha za umma, yanakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)," alisema.

Katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati kwa mwaka 2022/23, Bunge lilitaka serikali kuhakikisha TANAPA, NCAA na TAWA zinabakia (retain) na kiasi cha asilimia 30 ya makusanyo yao na kiasi kingine kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

Wakati anasoma taarifa hiyo, Mnzava ambaye pia ni Mbunge wa Korogwe Vijijini (CCM), alisema:

"Kwa kuwa hakuna mgogoro wowote wa mgawanyo wa fedha, kati Hazina na Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake, ambao ungepelekea kuanzishwa kwa akaunti hiyo;

"Na kwa kuwa kuanzishwa kwa akaunti hii kutapalekea matumizi ya fedha za umma kushindwa kufanyiwa ukaguzi na CAG, kwa utaratibu wa kawaida, Bunge linaazimia, serikali isitishe mara moja kuanzishwa kwa akaunti hiyo, hali inayoweza kupelekea fedha za umma kutumika bila usimamizi na uwajibikaji.

"Na serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Fedha Na. 8 ya Mwaka 2020 kwa lengo la taasisi hizi kubaki na sehemu ya makusanyo yake ili kuzisadia taasisi hizi kutekeleza majukumu yake ya uhifadhi kwa ufanisi."

Mnzava pia alisema Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) inapanga kuratibu uzalishaji wa filamu nne za kimataifa, zikiwamo mbili za mwendelezo wa Royal Tour na makala mbili za video za kimataifa kutoka kwa wazalishaji wa viwango vya Hollywood.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, moja ya filamu hizo itaitwa 'Kijiji cha Milele', iliyomshirikisha Rais Samia Suluhu Hassan na mwigizaji maarufu wa filamu, Jing Dong kutoka China.

Nyingine ni maandalizi ya makala inayohusu mchango wa Mwalimu Julius Nyerere katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Alisema mikakati yote hiyo inahitaji fedha nyingi, lakini kama taifa hakuna juhudi za makusudi katika kutangaza utalii ili kupata matokeo yanayotarajiwa.

Kuhusu hali ya utalii nchini, mwenyekiti huyo alisema hadi kufikia mwezi Desemba 2023, kwa taarifa za hali ya uchumi za robo ya mwisho ya mwaka jana, zinaonesha watalii walioingia nchini walikuwa 1,790,301 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kuwahi kufikiwa katika sekta hiyo.

Alisema sekta hiyo imeliingizia taifa fedha za kigeni zaidi ya Dola za Marekani bilioni 3.3, sawa na zaidi ya asilimia 25 ya mauzo yote ya nje nchini hadi kufikia Desemba 31, 2023.

Pamoja na mambo mengine, alisema sekta hiyo iliyoongoza katika kuingiza fedha za kigeni nchini, ikichangia zaidi ya asilimia 20 ya Pato la Taifa.

Kwa upande wa ajira, sekta hiyo alisema imeongeza ajira za moja kwa moja kufikia hadi ajira 1,600,000 sawa na asilimia 11 ya ajira nchini.

Miongoni mwa wageni waliotembelea Tanzania, asilimia 58 huvifikia vivutio vya hifadhi za taifa, na asilimia 42 hutembelea maeneo mengine ya utalii, ikiwamo NCAA na fukwe za Zanzibar.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD, IGALULA AUCTION MART AND COURT BROKERS, ASCERICS LTD,HOLLYNESS AUCTIONEERS, GADAU AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO.LTD,MCHINGA AUCTION MART ,JOMOK INVESTMENT CO.LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | MY WAY INTERNATIONAL SUPPLIES & ENT | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | ALLEN ADAM SANGA | UBUNGO SOUTH | 23/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | NEMONO LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NAMBA.40048 ,KIWANJA NAMBA 17&18 KITALU 'HHH' 2.SHAMBA EKARI 10 | TITUS RASHIDI MSHANA | SAME-KILIMANJARO | 23/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | REGINA CHARLES KAJOLE | NYUMBA | ATHUMAN RAJABU JONGO | KILUNGULE-MBAGALA | 14/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | JONATHAN ZAWADI MHANDO | NYUMBA | JONATHAN ZAWADI MHANDO | MBEZI MSAKUZI | 23/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MAFUBILLO GENERAL SUPPLIES LIMITED | NYUMBA | SEIF ALLY MUHERE | KAWE | 26/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | KASA MUSSA SELEMANI | NYUMBA | KASA MUSSA SELEMANI | CHANIKA | 16/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | AMOS MARWA NDEGE | NYUMBA | AMOS MARWA NDEGE | MSONGOLA-ILALA | 20/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MAX AYUBU MBONYE | NYUMBA | MAX AYUBU MBONYE | YONGWE-CHANIKA | 16/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | AGATHA PETER MREMA | NYUMBA | AGATHA PETER MREMA | KWEMBE-UBUNGO | 19/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | RAJAB IBRAHIM MBAMBWA | NYUMBA | RAJAB IBRAHIM MBAMBWA | KWA ALI MAUA-KIJITONYAMA | 16/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | SHEILA CLEVELAND NKATA | NYUMBA | SHEILA CLEVELAND NKATA | MBEZI LUIS | 22/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0787129539/0745707008/0743885084/0655715138/0692836202.
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



Mkurugenzi Mtendaji wa EATV/Radio, Regina Mengi, akizungumza na washiriki wakozi fupi ya uongozi kutoka vyama vya siasa, dini na asasi za kijamii inayoendeshwa na Chuo Cha Taifa cha Ulinzi, walipotembelea vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Picha zaidi Uk. 7. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Watembelea The Guardian kujifunza uzalishaji maudhui

**Na Jenifer Gilla**

VIONGOZI mbalimbali kutoka taasisi za dini, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya usalama na vyama vya siasa jana walitembelea Kampuni ya The Guardian kujifunza namna ofisi hiyo inavyofanya kazi na mchango wake katika kudumisha usalama wa nchi.

Mkuu wa Msafara huo, Brigedia Jenerali, Baganchwera Rutambuka, alisema viongozi hao ni washiriki wa kozi fupi ya 16 inayohusu uongozi inayotolewa na Chuo cha Taifa cha Ulinzi cha Dar es Salaam.

Alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza namna vyombo vya habari vinavyoshiriki katika kuimarisha usalama wa taifa kwa namna vinavyopeleka habari za viongozi kwa jamii, ili kuongeza uelewa wa namna demokrasia na vyombo vya dini vinavyochangia katika usalama wa taifa.

Alisema ni muhimu kwa viongozi hao kujua namna vyombo vya habari vinavyodumisha amani na demokrasia kwa kuwa wanavitegemea kupeleka taarifa zao kwa jamii.

"Usalama wa nchi si jambo la mtu mmoja, ni jambo la kila Mtanzania, kuanzia kwa viongozi na maelekezo wanayoyatoa kwa wafuasi wao na ninyi mnaosambaza, ndio maana tukaamua kutembelea kampuni hii," alisema.

Alisema chuo hicho kinafundisha kozi ndefu na fupi kuhusiana na usalama wa taifa, kozi fupi ni maalum kwa viongozi wakubwa ambao hawapati muda wa kuhudhuria mafunzo hayo kwa wiki 47 kutokana na majukumu yao.

Alisema lengo la kozi hiyo ni kuwajengea uwezo viongozi hao ili wakawe bora kwa kufanya kazi huku wakidumisha usalama wa nchi katika taasisi zao.

Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo, alisema magazeti ya The Guardian na Nipashe yanayozalishwa katika kampuni hiyo ni miongoni mwa vyombo vya habari vinavyoheshimika nchini kwa kutoa habari zenye uhakika.

Alisema suala hilo linawezekana kwa kuwa kampuni hiyo inafanya kazi kwa kuzingatia misingi ya taaluma, sheria za nchi na kuweka mbele maslahi ya jamii na ndio sababu kuu ya kuendelea kuwapo katika fani kwa miaka 30.

Alisema moja ya changamoto inayokumbana nazo kwa sasa ni kuanzishwa kwa vyombo vya habari vya mitandao vinavyosababisha biashara ya magazeti kuyumba, lakini wanakabiliana nayo kwa kushirikiana navyo kufanya kazi.

Alisema kwa sasa kampuni hiyo imeanzisha kitengo cha habari za mtandao ambazo nazo hutoa taarifa ili kuhakikisha wanawafuata wasomaji wao katika njia hiyo ya mawasiliano.

Mmoja wa viongozi wanaosoma kozi hiyo, Katibu Mkuu wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) Tanzania Bara, Eugene Kabendera, alisema kupitia ziara hiyo amejifunza umuhimu wa vyombo vya habari katika kudumisha usalama wa nchi.

Aliipongeza kampuni hiyo kwa kufanya kazi kwa uhuru na kuzingatia sheria na kuajiri vijana wengi, jambo linaloonesha kuwa ina mchango mkubwa katika kutoa ajira kwa kundi hilo.

# Utoaji wa mimba wachangia 10% vifo vitokanavyo na uzazi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel ameliambia Bunge kuwa utoaji mimba unachangia vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 10.

Alibainisha hayo jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Conchesta Rwamlaza. Mbunge huyo alihoji ukubwa wa tatizo la vifo vitokanavyo na utoaji mimba usio salama na madhara yake nchini.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema madhara yanayotokana na utoaji mimba usio salama ni pamoja na uambukizo mkali wa mfumo wa uzazi ambao unaweza kupelekea mgonjwa kutolewa mfuko wa uzazi na wakati mwingine kupoteza maisha.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kukabiliana na asilimia 10 ya vifo vya uzazi vinavyochangiwa na utoaji mimba usio salama.

Alisema serikali iliridhia Mkataba wa Maputo wa Nyongeza ambao ulikuwa unatetea haki za wanawake na afya, uzazi salama ukiwa sehemu ya mkataba huo.

"Makubaliano yalilenga kuhakikisha mimba zinazotolewa ni zile zinazopatikana kwa kubakwa, mashambulio ya kingono. Serikali haioni ni wakati kuridhia makubaliano ili kuwasaidia wanawake wanaopata mimba za aina hiyo kuzitoa kwa usalama bila kuhatarisha maisha yao?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Dk. Mollel alisema suala hilo ni muhimu kuzungumziwa ili kutoa elimu kwa wananchi kwamba kuna tatizo na watu wanapoteza maisha.

Alibainisha kuwa kwa mwaka, duniani mimba zisizo salama ni milioni 20 sawa na asilimia 13.

Alifafanua kuwa serikali itaendelea kutoa elimu ili kueleza watoto kuna wakati mwafaka wa kupata mimba na kujiepusha na mimba zisizo salama. "Inahitaji mchakato mkubwa kuruhusu mimba za namna hii kutolewa kwa kuwa ni suala linalohusisha wizara mbalimbali na imani za watu, tupeni muda tuendelee kuchakata ili tusizalishe tatizo lingine," alisema.

# Muhimbili yamwekea sehemu za siri za kike aliyezaliwa mvulana

**Na Pilly Kigome**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imefanya upasuaji kwa watoto 31 wenye changamoto mbalimbali za jinsi wakiwamo waliozaliwa na jinsi tata pamoja na upasuaji wa kipekee uliofanywa kwa mara ya kwanza wa kutengeneza jinsi ya kike kwa kutumia nyama za mwili.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam mbele ya waandishi wa habari.

Prof. Janabi alisema kati yao, sita walizaliwa na jinsi tata wakiwamo waliozaliwa na changamoto za kuzaliwa na tundu moja na changamoto za sehemu za haja kubwa na ndogo.

Alisema upasuaji wa kipekee uliofanywa kwa mara ya kwanza hospitalini huko ni ule wa kumwekea jinsi ya kike kijana aliyedhaniwa kuwa ni wa kiume mwenye umri wa miaka (24) ambaye alizaliwa na jinsi ya kiume, lakini baadaye ikagundulika jinsi hiyo haitakuwa na tija kutokana na uchunguzi wa kitabibu.

Alitaka watanzania kuwa makini na kuchunguza kwa umakini watoto pindi wanapozaliwa na wanapoendelea kukua kwa kuwa mtoto anaweza akaonekana ni wa jinsia ya kike kumbe ni wa kiume na anaweza akaonekana mtoto kiume kumbe ni wa kike.

"Pelekeni salamu kwa watanzania tayari Muhimbili tumeanza upasuaji wa kurekebisha jinsia, kuchunguza watoto na kubaini jinsia zenye nguvu, na tunaomba wazazi wachunguze watoto pindi wanapokabidhiwa ikiwamo kuchunguza tabia za watoto kadri wakuavyo.

"Unaweza ukamwona mtoto ni wa kike anapozaliwa, kadri anavyokuwa anakuwa na viashiria vya kiume au wa kiume anakuwa na mambo ya kike, basi fanya hima kufanya uchunguzi mara moja kwa vipimo, Muhimbili itagundua ni kwanini mtoto huyo ana tabia hizo, huenda vipimo vya kamera kwenye njia za uzazi na tumbo vitagundua," alifafanua.

Alifafanua upasuaji huo umefanyika kwa muda siku 21 kuanzia Januari 14 mwaka huu kwa wataalamu zaidi ya 20 kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Ireland na Jordan.

Daktari Bingwa Elekezi Upasuaji Watoto, Petronilla Ngiloi alisema upasuaji huo unajumuisha makundi makuu matatu, ukihusisha mkanganyiko wa utambuzi wa jinsia za watoto.

Alisema tatizo la kukanganya kwa makuzi ya watoto ni kilema kama vilema vingine na tatizo hilo linaweza likatokea kunapokuwa na muungano wa mbegu za kiume na kike kwa vinasaba vinavyotengeza utu wa binadamu.

Dk. Gabriel Mtaturu, Mbobezi wa Upasuaji Njia ya Mkojo, alisema takwimu zinaonesha kati ya watoto 5,000 wanaozaliwa duniani, mmoja anazaliwa na jinsi tata na kati ya watoto 300 watakaozaliwa, mmoja anazaliwa na changamoto ya kimaumbile.

Alisema kuwa kwa takwimu hizo, watanzania wanapaswa kuwa makini na kuwa na utaratibu wa kuchunguza makuzi ya watoto kwa kuwa mtoto anaweza akaonekana na kiume, lakini shida inakuja kadri akuavyo anakuwa na viashiria ambavyo vinaonesha si vya jinsia yake.

Aliwataka wazazi wote wenye shaka na ukuaji wa watoto wao kwenda kufanya uchunguzi na watagundulika kwa gharama nafuu ya kuanzia Sh. 300,000 hadi milioni 1.5.

## TANGAZO

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

"Kwa Maendeleo Yako"

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 12/31/22**
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | | Mwaka wa sasa 31/12/22 | Mwaka Uliopita 31/12/21 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 239 | 841 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 13 | 85 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 2,393 | 3,215 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 15,641 | 15,051 |
| 12 | Mali nyingine | - | 4,528 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 3,738 | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 514 | 569 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **22,538** | **24,289** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 1,003 |
| 18 | Amana za Wateja | 14,060 | 15,269 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 86 | 138 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 186 | 536 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 503 | 472 |
| 28 | Madeni | 3,776 | 2,527 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **18,614** | **19,945** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **3,924** | **4,344** |
| | | | |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5,724) | (5,274) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 181 | 716 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 677 | 113 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **3,924** | **4,344** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,020 | 1,843 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 191 | 815 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 9.87% | 16.14% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 111.24% | 13.20% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 69.40% | 92.45% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 84.61% | 60.98% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | -13.78% | 85.00% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -7.21% | 4.20% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -7.21% | 34.47% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**
**KWA MWAKA INAYOISHIA 31-12-2022**
**(Kiasi cha shilingi milioni)**

| | | Mwaka wa Sasa 12/31/22 | Mwaka Uliopita 12/31/21 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,014 | 4,151 |
| 2 | Gharama za Riba | (734) | (665) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 2,280 | 3,486 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (190) | (374) |
| | | | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 890 | 550 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 890 | 550 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | **(2,793)** | (2,763) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,243) | (1,175) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (54) | (54) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,496) | (1,534) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | 187 | 899 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (6) | (157) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | 181 | 742 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | 181 | 742 |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 56 | 54 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 5.54 | 23 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 1.51% | 3.84% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 4.75% | 19.48% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 76.41% | 66.73% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 5.33% | 21.87% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho**

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA**
**KWA MWAKA INAYOISHIA 31-12-2022**
**(Kiasi cha shilingi milioni)**

| | | Mwaka wa Sasa 31/12/22 | Mwaka Uliopita 31/12/21 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 187 | 899 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | Hasara Katika Mali | 409 | 574 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (780) | (1,462) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (2,260) | 1,211 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (334) | (115) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 412 | (972) |
| | Kodi Iliyolipwa | (120) | (239) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **(2,486)** | **(104)** |
| | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | - | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (195) | (117) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(195)** | **(117)** |
| | | | - |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **(1,400)** | (260) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | **2,650** | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | **(65)** | (91) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **1,185** | **(351)** |
| | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | (1,496) | (572) |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Mwaka | 4,141 | 4,713 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Mwaka | **2,645** | **4,141** |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31-12-22**
**(Kiasi cha shilingi milioni)**

| | | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mwaka wa sasa** | | | | |
| | **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,344** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 181 | - | **181** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| | Miamala na Wanahisa | (4) | - | - | **(4)** |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| | Ziada ya Kisheria | - | (568) | 568 | **-** |
| | Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | **-** |
| | Mengineyo | - | (598) | - | **(598)** |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,791** | **(5,543)** | **675** | **3,923** |
| | | | | | |
| | **Mwaka Uliopita** | | | | |
| | Salio la mwanzo wa mwaka | **8,886** | **(5,280)** | **87** | **3,693** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 742 | - | **742** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| | Miamala na wanahisa | (91) | - | - | **(91)** |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| | Ziada ya Kisheria | - | (20) | 20 | **(0)** |
| | Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | **-** |
| | Mengineyo | - | - | - | **-** |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,344** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAYOISHIA 31- 12-2023

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Philipo Raymond<br>Meneja Mkuu | ........................................ (Imesainiwa) | 31/01/2024 |
| Kelvin Mushi<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | ........................................ .... (Imesainiwa) | 31/01/2024 |
| Saleh S Abdallah<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | ................................................ (Imesainiwa) | 31/01/2024 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | Tarehe |
|---|---|
| 1. Bakar R. Bakar.........................................................(Imesainiwa)<br>Mkurugenzi | 31/01/2024 |
| 2. Prof. Dominicus Kasilo.........................................(Imesainiwa)<br>Mkurugenzi | 31/01/2024 |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# SMZ iingilie kati sakata la vileo kuokoa sekta ya utalii

**KWA** muda wa wiki kadhaa sasa, kumekuwa na mjadala na malalamiko kuhusu kuadimika kwa vileo husuan pombe kali Zanzibar hali ambayo inaelezwa kuwa inaweza kuathiri sekta ya utalii ambayo ni mhimili mkuu wa uchumi visiwani humo.

Sakata hilo lilianza mwanzoni mwa mwaka huu baada ya Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar kudaiwa kuwapa vibali waagizaji wapya ambao si Wazanzibari huku ikiwaengua waliokuwa wakifanya shughuli hiyo.

Jambo hilo liliibua mjadala wa kisiasa likihusisha pia kujiuzulu kwa aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, kwa kile kilichodaiwa kuwa aliamua kufanya hivyo kutokana na mazingira yasiyo rafiki katika kutekeleza majukumu yake.

Kwa sasa suala hilo limeendelea kuchukua uzito katika mijadala ya kisiasa na kijamii na kuwaibua watu mbalimbali kutoa maoni yao huku lawama nyingi zikiiendea serikali kwa kushindwa kulisimamia ipasavyo. Juzi, mathalani, wanasiasa na wanaharakati waliibuka na kuitupia lawama Bodi ya Udhibiti wa Vileo kwamba ni chanzo cha tatizo hilo kwa madai ya kuvunja Sheria ya Udhibiti wa Vileo ya mwaka 2020.

Kifungu cha 33 cha sheria hiyo, kwa mujibu wa wanasiasa na wanaharakati hao, kama ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wanaopaswa kupewa leseni kwa ajili ya kuagiza bidhaa hiyo ni watatu na sharti la kupewa ni lazima wawe Wazanzibar lakini inadaiwa sheria hiyo imekiukwa kwa bodi kuwapa watu ambao hawakidhi vigezo kwa maana si Wazanzibari.

Asilimia kubwa ya uchumi wa Zanzibar, unategemea utalii kutokana na kuwapo kwa fukwe nzuri na maeneo ya kale ambayo huwavutia wageni wengi kutoka mataifa ya nje. Sekta hiyo pia imevutia wawekezaji wengi wa hoteli na maeneo ya starehe ambayo pia huuzwa pombe. Kwa mantiki hiyo hiyo, kukosekana au kuadimika kwa pombe katika hoteli nyingi na sehemu za burudani, kunatia doa sekta ya utalii na uchumi kwa ujumla kwa kuwa kupitia vinywaji kodi ya serikali inapatikana. Kutokana na ukweli huo, ni vyema serikali ikaingilia kati suala hilo na hatimaye bidhaa hiyo ikapatikana kwa wingi katika hoteli za kitalii kama ilivyokuwa awali na pia kuondoa mgogoro uliopo ambao umegeuka na kuwa siasa.

Kama ilivyoshauriwa na baadhi ya wadau, ni vyema sheria inayosimamia uagizaji wa vileo visiwani humo ikasimamiwa ipasavyo kwa kuwapatia vibali watu wenye sifa tofauti na inavyodaiwa jambo ambalo pia linahusisha kuwapo kwa harufu ya rushwa. Inadaiwa kuwa waliokuwa wakifanya biashara hiyo kwa zaidi ya miaka 30 wameenguliwa na kupewa watu wasio na uzoefu, hivyo kusababisha kuwapo kwa tatizo katika biashara ya vileo Zanzibar.

Pamoja na kufuata masharti hayo kama ilivyoainishwa katika sheria, ni wakati mwafaka sasa sheria hiyo pia kufanyiwa mabadiliko kwa kuweka mipaka ya kibiashara kwa kutaka kuwapo watu watatu tu katika kufanya biashara hiyo.

Katika ulimwengu wa sasa, uchumi wa dunia umehama kutoka hodhi na kuwa wa soko ambao unaruhusu uwanda mpana wa watu kufanya biashara kwa ushindani huku serikali ikiweka sheria, miongozo na taratibu katika kufanikisha azma hiyo. Kwa mantiki hiyo, watu wenye uwezo katika biashara fulani, wanaruhusiwa kufanya kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa huku serikali ikiwa msimamizi wa sheria.

Kutokana na hali hiyo, ni wakati mwafaka kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kufanya marekebisho ya sheria ya udhibiti wa vileo ili kutoa nafasi kwa watu wengi zaidi kushiriki huku ikisimamia kanuni na taratibu katika kuhakikisha hakuna anayevunja sheria wala miiko na utamaduni wa visiwa hivyo ambavyo kwa kiwango kikubwa vinatawaliwa na Imani ya dini ya Kiislamu.

Aidha, kuwapo kwa mazingira ya rushwa katika utoaji wa vibali vya sasa vilivyosababisha kuwapo kwa uhaba, taasisi zinazoshughulikia masuala hayo zifanye kazi na iwapo itabainika kuwapo kwa mazingira hayo, basi serikali iwawajibishe na sheria ichukue mkondo wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Dai la uzoefu, linawaweka pagumu wahitaji waajiriwa wanaotoka shule

**"NI** kweli hapa nafasi za kazi zinapatikana, lakini hapa tunahitaji watu wenye uzoefu wa kuanzia miaka miwili na kuendelea." Hii ni moja kati ya kauli zinazotumiwa na waajiri mbalimbali katika sekta binafsi na serikalini, pindi mtu anapoomba kazi.

Ukweli usiopingika, kauli hiyo imekuwa ikiwafanya baadhi wa wasomi Katika fani mbalimmbali kukosa ajira, licha ya kuwa na elimu, kigezo cha uzoefu kikawa kipingamizi Katika kupata ajira.

Ukiliangalia hilo kwa upana wake, unagundua wazazi wamewekeza pesa na nguvu kubwa ili kuwasomesha Watoto, baadae wakiajiriwa waje kuisaidia familia zao na taifa.

Lakini, upande wa pili wa sarafau, kitendo cha kuhitaji watu waliosoma na wenye uzoefu wa kazi zaidi ya miaka miwili, hilo siyo jambo jema na ni kitu cha kupigiwa kelele.

Hapa ninajiuliza swali, katika hali ya kawaida mtu aliyemaliza chuo labda kwa ngazi ya shahada anataka ajira halafu anaambiwa mpaka awe na uzoefu na baadae mtu huyo anakosa kazi, licha ya kuwa na elimu yake, hivi huko ni kujenga au kubomoa?

Nimeona niulize hilo, kwa sababu kama elimu aliyoipata mwanafunzi chuoni inajitosheleza kwa mtu kufanya kazi, na hasa sasa suala la mwenye uzoefu linatoka wapi?

Wakati mwingine inauma sana kwa wazazi wanaposikia mwanae alimsomesha pengine kwa kujidhiki, akafaulu vizuri akakosa kazi kisa hana uzoefu wa kazi anayoomba.

Sasa swali la kujiuliza, kama huyu ameomba nafasi ya kazi Katika kampuni halafu akanyimwa ajira kwa kuwa ameonekana hana uzoefu huyu mtu sasa uzoefu ataupata wapi kama kakosa nafasi ya kuajiriwa ili apate uzoefu?

Labda kwa leo nitumie ukurasa huu kuuliza hivi, kati ya uzoefu na elimu, kipi ni kitu muhimu cha msingi kwa mhitaji wa ajira, vilevile hata mwajiri?

Suala hili limekuwa gumzo sana mitaani, hasa kwa wanafunzi wanapomaliza vyuo, wanapoenda kuomba ajira na kukutana na kasumba hiyo. Kuna haja ya mamlaka husika kuliangalia suala hilo kwa mapana na kuona namna ya kumsaidia mtu kupata ajira hata Kama hana uzoefu wa kazi hiyo ili mradi tu awe amesomea hicho kitu.

Waswahili walisema 'mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe', sasa huyu maskini ameshasoma tayari hiyo ndio nguvu yake, lakini kwenye kusaka ajira anakutana na kigezo ambacho pengine hakuwahi kukitarajia Katika harakati zake za masomo.

Ombi langu kwa serikali, ilitazame suala hilo kwa undani, ili kupunguza changamoto katika usakaji wa ajira kwa wahitaji, ili kusudi kama wanapata ajira wapate ajira kulingana na taaluma yake na sio kukosa ajira kisa amekosa uzoefu.

Wahenaga waliwahi kusema "chovya chovya humaliza buyu la asali" maana ni kwamba, kama hili suala halitapigiwa kelele mapema baadae itakuwa mtu haajiriwi licha ya kuwa na elimu kwa kukosa uzoefu, ni vema samaki huyu akunjwe angali mbichi ili kusaidia wahitaji wa ajira kupunguziwa vipingamizi.

Wakati mwingine unaweza kujiuliza Kama mtu ananyimwa ajira, kisa uzoefu wakati kazini ndio mahari pakupatia uzoefu sasa waliopo hapo kazini walipata uzoefu wapi?

Nani atakubali kumuajiri mtu asiye na uzoefu? nawaliaminikaje ikiwa hawana uzoefu au labda Kuna kigezo nje ya elimu ambacho kinaangaliwa pengine yawezekana wengi wao hawana! au shida ipo wapi Katika hilo?

• Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa namba 0787879707

HABARI PICHANI

# Ziara ya Chuo cha Taifa cha Ulinzi katika vyombo vya habari vya IPP



Mmoja wa wakufunzi kutoka chuo hicho, Brigedia Jenerali Baganchwera Rutambuka, akikabidhi zawadi ya kalenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile.



Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo, akifafanua kuhusu utendaji kazi wa chumba cha habari cha magazeti ya The Guardian na Nipashe.



Mkurugenzi Msaidizi wa Capital Radio, Bahati Alex, akielezea kuhusu urushaji wa vipindi katika radio hiyo.



Mhandisi wa kiwanda cha uchapaji wa magazeti cha The Guardian Ltd, Christian Ngwapaula (katikati), akifafanua jambo kuhusu kazi ya kiwanda hicho. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**



Baadhi ya washiriki wa kozi fupi ya Uongozi na Usalama wa Taifa wakiwa katika moja ya studio za ITV.



Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/RADIO ONE, Joyce Mhavile, akielezea jinsi vipindi vinavyorushwa.

# Morogoro kuvuna maji ya mvua kukabili mafuriko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima amesema mkoa huo umewasilisha mapendekezo Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kusaidia kudhibiti maji ya mvua yanayosababisha mafuriko.

Udhibiti huo umelenga kuyavuna maji kwa kuhifadhi kwenye mabwawa ili yatumike kwenye shughuli za kijamii na kiuchumi.

Malima aliyasema hayo wakati wa maadhimisho ya kumbukizi ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM), Februari 5, 1977 yaliyofanyika kimkoa mjini Morogoro, mgeni rasmi akiwa Mlezi wa CCM mkoani na Mwenyekiti wa Taifa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM), Mohamed Ally Kawaida.

Alisema kutokana na mafuriko yaliyojitokeza hivi karibuni na kuleta madhara, serikali ya mkoa imepeleka mapendekezo kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhangama alipofika mkoani Morogoro kujionea hali halisi ya athari za mafuriko yaliyosababisha madhara kwa wananchi.

"Mvua iliyosababisha mafuriko katika miaka miwili ya hivi karibuni imekuwa ikiongezeka kwa kasi sana kwenye wilaya zote za Mkoa wa Morogoro, zimeathirika na mafuriko na imetokea kwa siku moja wilaya karibu nne zilikubwa na mafuriko," alisema Malima.

Mkuu wa Mkoa alisema mafuriko hayo yameleta athari ya mali, mashamba yenye mazao na kupoteza uhai wa binadamu kwa kiasi kikubwa.

Malima alisema kwa ujumla katika mafuriko yote hayo kwa miezi mitatu iliyopita, mkoa umepoteza karibu watu 20.

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imepanga kugharamia mafunzo ya muda mfupi ya ujuzi wa uokoaji kwa vijana zaidi ya 74 wa Fire Volunteer ambayo yatapangwa siku za usoni kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro.

Malima alisema hayo alipokabidhi fedha Sh. milioni 1.6 kwa vijana hao ikiwa ni kutimiza ahadi yake kutokana na kazi kubwa walioifanya ya kujitolea kwenye uokoaji watu na mali nyakati za mafuriko ya Januari 25, mwaka huu yaliyotokea maeneo mbalimbali ya mkoa ikiwamo Manispaa ya Morogoro.

"Kwenye mafuriko ya siku ile pale nikakuta kuna watu Volunteers wa zimamoto na uokoaji wa kujitolea lile jambo binafsi likanipa faraja kubwa nilisema nitatoa Sh. milioni moja mkapate hata sabuni kwa wale vijana 33 waliokuwapo pale," alisema.

Malima alisema vijana hao wanaojitolea katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wameiounga mkono uokoaji watu na mali zao baada ya kutokea mafuriko ya Januari 25, 2024 katika Manispaa ya Morogoro.

Mkuu wa Mkoa pia aliwaasa vijana hao kuwa na nidhamu, maadili mema, utayari na kutambua kuwa jambo hilo ni la kujitolea hususan katika kipindi chote watakachokuwa kwenye mafunzo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Shabani Marugujo alisema lengo la kuanzisha askari wa kujitolea wa Zimamoto na Uokoaji (Fire Volunteers) ni kutokana uwezekano wa kutokea kwa majanga ya moto na mafuriko.

Marugujo alisema majanga hayo yanasababishwa na kukua kwa teknolojia, ongezeko la watu na ukuaji wa miji na mabadiliko ya tabianchi, hivyo ni muhimu vijana hao kuwa nao ili kuongeza nguvu katika uokoaji.

## Bil. 38/- zahitajika ujenzi nyumba za walimu nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imefanya tathmini ya maboma ya nyumba za walimu na darasa yaliyoko kwenye maeneo mbalimbali nchini na kubaini Sh. bilioni 38.03 zinahitajika ili kukamilisha ujenzi wake.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi alibainisha hayo jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM,) Asha Abdullah Juma.

Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kuhusu maboma ya majengo ya nyumba za walimu na madarasa yaliyotelekezwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi alisema serikali imefanya tathmini ya maboma ya nyumba za walimu ambapo jumla ya maboma 2,527 yamebainishwa.

"Ili kukamilisha maboma haya, zinahitajika Sh. bilioni 37.905 na kila boma litagharimu Sh. milioni 15. Kwa upande wa madarasa, jumla ya maboma ya madarasa 10,106 yanayohitaji Sh. milioni 126.6 yametambuliwa," alisema.

Alieleza kuwa serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya nyumba za walimu na madarasa yaliyoanzishwa na wananchi.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Thea Ntara, alihoji sababu za serikali kutotoa fedha haraka kukamilisha maboma hayo.

"Kwa kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa madarasa, serikali ina mpango gani kuwa na mkakati wa kudumu ili hali hiyo isijitokeze tena?" alihoji.

Ndejembi akijibu maswali hayo, alisema katika sera ya ugatuaji madaraka, jukumu la kujenga miundombinu yoyote ya maendeleo katika halmashauri ni la wananchi, na serikali kuu imekuwa ikifanya usimamizi.

Alisema ni jukumu la mkurugenzi kutenga fedha lakini serikali kuu itaendelea kutafuta fedha kukamilisha maboma na madarasa mapya.



Mhandisi Mwandamizi anayesimamia ubora na viwango katika miradi ya kampuni ya GGML, Maftah Seif (kulia) akitoa taarifa kwa Ofisa Mkuu wa Masuala ya Fedha kutoka AngloGold Ashanti ambayo ni kampuni mama ya GGML, Gillian Doran kuhusu maendeleo ya mradi wa kuingiza umeme wa TANESCO katika mgodi wao, jana. Wengine ni maofisa waandamizi wa AngloGold Ashanti na GGML. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme mgodini wafikia 95%

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

JITIHADA za Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kuanza kutumia umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), zimezidi kuonekana baada ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme na mradi wa kupeleka umeme katika mgodi huo kufikia asilimia 95.

Kituo hicho kinachojengwa kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 24.4, kitakuwa na uwezo kupooza umeme wa msongo wa Kilovolt 33 kuwa Kilovolt 11 ndani ya mgodi wa GGML na kina uwezo wa Megawatt 40.

Akitoa taarifa wiki iliyopita mkoani Geita kwa Ofisa Mkuu wa Masuala ya Fedha kutoka AngloGold Ashanti ambayo ni kampuni mama ya GGML, Gillian Doran, Mwandamizi anayesimamia ubora na viwango katika miradi ya kampuni hiyo, Maftah Seif alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika katikati ya mwezi ujao kulingana na hali ya upatikanaji umeme wa TANESCO.

Alisema kazi kubwa iliyobaki sasa ni kukamilisha ufungaji mifumo ya mitambo hiyo pamoja na kuanza majaribio ya mitambo hiyo katika kituo hicho.

Akifafanua zaidi kuhusu mradi huo, Makamu Rais wa AngloGold Ashanti anayeshughulikia miradi endelevu na masuala ya ubia/ushirika Afrika, Simon Shayo alisema TANESCO hivi karibuni walikamilisha ujenzi wa laini ya kilovolt 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita huku ujenzi wa laini ya kilomita sita yenye kilovolt 33 kuelekea katika mgodi wa GGML ukiwa katika hatua za mwisho.

Alisema licha ya kwamba kampuni nyingi za madini tangu miaka ya 2000 hutumia umeme wanaouzalisha wenyewe, sasa serikali imekuwa na jitihada za makusudi kufungamanisha sekta ya nishati na sekta kubwa za uzalishaji kwa kuzalisha umeme unaotosheleza mahitaji ya wawekezaji wakubwa.

"Sisi kwa sekta ya madini tunaona hii kama ni baraka kubwa kwa sababu huwezi kuendesha migodi mikubwa kama ya kwetu (GGML) kwa kutumia jenereta," alisema. Alitoa mfano kuwa GGML hutumia Megawati 40 ambazo huzalisha kwa mafuta ya dizeli, lakini sasa wanatamani kuona mradi wa kupeleka umeme wa TANESCO katika mgodi wa kampuni hiyo ukikamilika ili kupunguza gharama za uendeshaji.

"Tukijiunga tu na TANESCO kwenye Gridi ya Taifa na kutoka kwenye umeme tunaouzalisha wenyewe, tutapunguza gharama za umeme kwa asilimia 50, tutaokoa Dola za Marekani milioni 19 kila mwaka. Pia tutapunguza hewa ya ukaa kilotons 81 kufikia mwaka 2030," alisema.

Aliongeza kuwa nchi iko katika mipango ya kuwekeza pakubwa katika sekta ya madini kwa kuanzisha migodi ya uzalishaji madini mengine sehemu mbalimbali nchini, hivyo ni dhahiri kuwa TANESCO itafanikiwa kuongeza mapato makubwa kutokana na mchango wa migodi hiyo kwenye matumizi ya umeme.



# Wanawake wamwomba polisi simu washtaki waume zao

**Na Steven William ,** MUHEZA

WANAWAKE wa kitongoji cha Kwegole Kijiji cha Mikwamba Kata ya Magila wilayani hapa Mkoa wa Tanga, wametoa mpya baada ya kumuomba namba ya simu askari polisi wa kata hiyo kwa lengo la kuwashtaki waume zao kwa tuhuma za unyanyasaji wa kijinsia.

Tukio hilo lilitokeza juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kitongoji hicho na kuhudhuriwa na askari huyo wa Jeshi la Polisi Kata ya Magila, Mkaguzi Frank Mwemsi.

Wanawake hao walitumia fursa hiyo kuomba namba ya simu baada ya Mwemsi kutoa elimu juu ya kupinga unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Akitoa elimu hiyo, alisema wananchi watambue kuwa jeshi hilo sio adui, wanapaswa kuwa marafiki kwa kuwasilisha malalamiko yao dhidi ya ukatili wa kijinsi wanaofanyiwa na waume zao ili kutokomeza vitendo hivyo katika jamii.

Mwemsi, alisema wananchi pia wanatakiwa kutoa taarifa za matukio wanayoshuhudia ya uhalifu katika maeneo, yakiwamo ya wizi na uuzaji wa dawa ya kulevya ili kukomesha vitendo hivyo.

Aliwakumbusha wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu na macho ambao umeyakumba maeneo mengi nchini ikiwemo Muheza na kuwahimiza wazazi kupeleka watoto wao shule mwaka huu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kwegole, George Sakala, alisema wakazi wa kitongoji hicho lazima wajenge utamaduni wa kushiriki nguvu kazi na asiyetaka ahame, lasivyo atakamatwa na kupelekwa Ofisi ya Ofisa Mtendaji Kata kujibu mashtaka.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Rose Mdaki aliomba apelekewe orodha ya majina ya wakazi hao ambao hawataki kuchangia nguvu kazi ili washtakiwe na kutozwa faini.



Mkazi wa wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Ramadhani Husseni akifanya biashara ya kukuna nazi kwa mashine maalum katika eneo la Amtico Relini ambapo nazi moja anakuna kwa 100/-. Kushoto ni mteja akisubiri kupatiwa huduma hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# 'Majengo hayana miundombinu ya walemavu'

**Na Mary Mosha MOSHI**

ASILIMIA 70 ya miundombinu ya majengo nchini haijajengwa kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu na kusababisha kundi hilo kujiona wamebaguliwa.

Akizungumza na Nipashe, Rais wa Shirika la New life Foundation, Askofu Glorious Shoo alisema kuwa hayo yamebaini katika utafiti uliofanyika kwenye makanisa, shule, hoteli, kumbi za starehe, taasisi za serikali, binafsi na nyumba za watu binafsi.

Askofu Shoo alisema hivi karibuni wanatarajia kutangaza siku ya watu wenye ulemavu ikiwa ni sehemu ya kurudisha walichopata kwa jamii.

Alisema wanahimiza kukumbusha kila mara katika jamii kunapofanyia ujenzi au ukarabati wa majengo kuwekwa maeneo au mifumo kwa ajili watu hao wenye ulemavu.

Mratibu Mafunzo na Uendeshaji wa Shirika hilo, Gerald Simon, alisema wanatarajia kuwakutanisha watu wenye ulemavu zaidi 60 wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya kusherehekea siku hiyo ili kuwaonyesha ambavyo wanatambulika na kuheshimika kwenye jamii.

"Siku hiyo tutakuwa na usiku wa kupendeza, watu wenye ulemavu tutawaonyesha tunawatambua na tunawathamini na wanapaswa kupewa kipaumbele kama ilivyo kwa watu wengine," alisema.

# UDOM yajivunia 'kuwapika' vijana kwa utafiti

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Rose Joseph amesema wanajivunia vijana chuoni hapo kwa kufanya vizuri nchini na duniani katika utafiti na bunifu zenye kutatua changamoto kwenye jamii.

Akizungumza jana jijini Arusha katika maonyesho yanayofanyika Viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC), Rose, alisema UDOM wanawandaa wanafunzi wao kujitegemea na kujiajiri kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Hapa chuo tumekuwa mbele kushirikiana na serikali mtandao (eGA) kwenye eneo zima la TEHAMA na tuna wanafunzi wengi waliobuni vitu vyenye manufaa kwa jamii. Kama hapa sasa tuna mwanafunzi amebuni mfumo 'application' utakaowezesha vijana wenye mawazo ya kibiashara kupata ufadhili wa kifedha duniani," alisema.

Alisema kuna mwingine amebuni mfumo wa kielekroniki unaohifadhi taarifa za biashara na mfumo bandia unaosaidia kutoa tathimini ya biashara inapofanya vizuri au vibaya na kushauri njia sahihi ya kukuza biashara.

Alisema lengo la chuo hicho ni kuzalisha wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa kufanya tafiti na bunifu zenye tija kwa Taifa na kuwawezesha vijana wao kukubalika katika soko la ajira duniani.

Rose, alisema chuo hicho kinafanya vizuri kwenye masuala ya TEHAMA na kwamba hivi karibuni kimeshinda shindano kubwa lililoandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa wanafunzi wao watatu kuibuka kidedea nafasi ya kwanza hadi ya tatu.

Alisema hata katika mashindano mengine ya masuala ya TEHAMA barani Afrika na duniani, wamekuwa wakishinda.

Alisema wameadhamiria kushirikiana na wadau kutumia vijana wenye bunifu zao kuwasaidia ili zilete manufaa kwa Taifa na kwao kiuchumi.

Mwanafunzi wa UDOM, Ipyana Mwampeta, alisema amebuni mfumo wa kusaidia wenye mawazo ya kibiashara wapate ufadhili duniani, baada ya kubaini vijana wengi wana mawazo mazuri ya kibiashara lakini hawana nguvu ya kifedha.

"Vijana wengi wakibuni mawazo yao ya kibiashara wanaweza kuwa na mawazo mazuri, lakini hawana nguvu ya fedha ila kupitia mfumo au application hii itawasaidia kupata ufadhili duniani. Ombi langu watakaopata fedha wazitumie kufanya kazi iliyokusudiwa," alisema.

# Madiwani sasa waiangukia serikali kausha damu

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wameiomba Serikali kurejesha mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani kuinusuru jamii kudidimia kiuchumi kwa kujiingiza kwenye mikopo ya umiza na kausha damu kwa riba kubwa.

Mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani, ilikuwa inatolewa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, mwaka jana ilisitishwa na serikali baada ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuonyesha kuwapo kwa upotevu wa mamilioni ya fedha kwenye mikopo hiyo.

Diwani wa Viti Maalum, Paulina Makeseni, akizungumza kwenye kikao cha baraza la madiwani la halmashauri hiyo, alisema jamii imejiingiza kwenye mikopo umiza na kausha damu na kutaabika kwenye urejeshaji.

Makeseni, aliiomba serikali kurejesha mikopo hiyo ili kuinusuru jamii kwa kuwa imejiingiza kwenye taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa riba kubwa.

Diwani wa Endiamtu, Lucas Zacharia, alisema kwa kipindi hiki jamii inapitia kwenye wakati mgumu baada ya kukosa fedha za mikopo hiyo ya serikali kwani zilikuwa zikiwasaidia kabla ya kusitishwa.

Alisema baada ya mikopo hiyo kusitishwa wananchi hasa wanawake wamejiingiza kwenye umiza na kausha damu na kudidimia kiuchumi.

"Hizi taasisi za fedha zimesababisha wananchi wangu kuingia kwenye tafrani kwa kuwa wengine wamenyang'anywa samani za ndani walizoweka dhamana kuchukua mikopo hiyo," alisema Zacharia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gracian Makota, alisema serikali haijarejesha mpango wa utoaji mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Makota, alisema endapo mpango huo utarejeshwa viongozi wa siasa wanapaswa kuwapa msukumo waliokopa warejeshe ili wengine wapate fursa hiyo.

Alisema mtu mwenye akili timamu akichukua mkopo anapaswa kurejesha na siyo kutetewa ili asirejeshe jambo ambalo siyo sahihi na kuwataka wajirekebishe.

"Kuhusu suala la taasisi za fedha kutoa mikopo na kunyang'anya vitu walivyoweka dhamana ikiwemo televisheni au chochote tumefuatilia na wamekanusha kukamata hivyo vitu," alisema Makota.





# Kiama wahalifu mitandaoni chaja

**Na Remmy Moka, SAUT**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema Serikali iko katika mkakati wa kuimarisha ulinzi mitandaoni ili kudhibiti vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na baadhi ya watumiaji kutoa lugha za matusi na kupotosha jamii.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Mkurugenzi wa Idara ya Leseni na Ufuatiliaji wa TCRA, John Daffa katika Maadhimisho ya Siku ya Usalama Mtandaoni kwa mwaka huu yaliyofanyika jijini hapa.

Akizungumza na wanafunzi wa vyuo na wadau mbalimbali, alitaja vitendo hivyo ambavyo vimeanza kukithiri katika mitandao iyo kuwa ni wizi, matusi na uvunjifu wa maadili unaofanywa baadhi ya watumiaji na kuitaka jamii kubadilika

Alisema taasisi za umma na binafsi, wanafunzi, wadau na jamii wanatakiwa kuhakikisha matumizi ya mtandao yanakuwa na manufaa kwa maslahi ya taifa na si vinginevyo.

Daffa, alisema kwa sasa mitandao inatumiwa kwa asilimia kubwa nchini kama chanzo cha kukithiri kwa uhalifu na uvunjifu wa maadili katika jamii hususani kwa wanafunzi wa shule hadi vyuoni.

Alisema kuna haja ya kueleekeza nguvu kudhibiti matumizi yasiyofaa ya mitandao ili kujenga jamii yenye manufaa kwa taifa la sasa na baadaye.

"Jamii inatakiwa kutambua kuwa matumizi mabaya ya mitandao ni kinyume na maadili,tumejipanga kuboresha ulinzi kwa watumiaji na hatua kali zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wahalifu husika,"alisema Daffa.

Kuhusu watumiaji wa mitandao nchini, alisema katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana wameongezeka kwa asilimia 4.1, idadi kubwa ikiwa nivijana.

Baadhi ya washiriki wa maadhimisho hayo, waliiomba TCRA kuongeza nguvu kudhibiti vitendo hivyo vya uhalifu kwa kutoa elimu kwa watumiaji na kutoa adhabu kali kwa wanaokiuka sheria.

"Wapo wanaotumia mitandao kuchafua watu na kuzusha taarifa za uongo, ipo haja kwa mamlaka kufanya jitihada kuwabaini kwa lengo la kukomesha vitendo visivyofaa ndani ya jamii,"alisema Zakia Abdul.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Simioni Kiles (katikati), akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo, lililokutana kupendekeza makadirio ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025, juzi. Kushoto ni Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara. **PICHA: TIMOTHY ITEMBE**

# Televisheni 'darasa' yatolewa vituo vya afya

**Na Vitus Audax,MWANZA**

TELEVISHENI 57 zimetolewa kwa vituo vya afya vya mikoa mitano nchini kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi ya kuepuka na kudhibiti magonjwa ya milipuko katika maeneo yao.

Televisheni hizo zimetolewa na Wizara ya Afya na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa vituo hivyo vilivyopo mikoa ya Mwanza,Geita,Shinyanga,Simiyu,Kagera na Singida.

Akizungumza wakati wa kukabidhi televisheni hizo juzi mkoani hapa, Ofisa Programu wa Mawasiliano ya Afya wa Wizara hiyo, James Mhitu, alisema lengo ni kuelimisha jamii jinsi ya kuepuka magonjwa hayo na mengine hususan ya milipuko.

"Katika eneo la kusubiria huduma ni sehemu pekee ambayo tumeona tunaweza kumfikishia mwananchi elimu namna ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali,"alisema Mhitu.

Alisema Wizara hiyo imepamga kupeleka televisheni kwa vituo vyote vya afya nchini kwa ajili ya kuelimisha wananchi na kuhasisha kupima afya kwa hiari.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk.Thomas Rutachunzibwa, alisema televisheni hizo zitakuwa msaada wa kukabiliana na magojwa ya mlipuko kikiwemo kipindupindu ambao umeendelea kusambaa mkoani hapa.

"Hii ni sehemu muhimu katika kudhibiti maambukizi magonjwa ya mlipuko na ni mkakati wa kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii katika maeneo muhimu,"alisema Dk.Rutachunzibwa.

Mwakilishi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Florah Kajumla, aliahidi televisheni hizo kutunzwa na kutumika kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii.

Ofisa Uhusiano wa REA, Jaina Msuya, alisema katika mapambano dhidi ya magonjwa ya milipuko wakala huo, umeendelea na mikakati ikiwemo kupeleka huduma ya umeme katika zahanati na vituo vya afya vijijini na maji safi na salama kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) ili kuboresha huduma.

"Huduma hizo zitawapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu wananchi kufuata huduma zinazohitaji umeme na kupunguza vifo visivyo vya lazima, televisheni hizi zitawasaidia kuelimika dhidi ya magonjwa yatakayokuwa yakitangazwa,"alisema Jaina.

# DC Mboni aweka kambi ofisini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita ameweka kambi ofisini kwake kusikiliza na kutatua kero zinazowakibili wananchi.

Akizungumzia kuhusu kambi hiyo, Mboni, alisema ni ya siku tatu kuanzia Februa 6 hadi 9, mwaka huu.

Alisema katika kambi hiyo, atasikiliza kero za wakazi wa kata 58 za Halmashauri ya Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama na kuzipatia ufumbuzi papo hapo.

Alisema katika kambi hiyo, imeibainika kuwa maeneo mengi ya kata hizo yanakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi, ikilinganishwa na sekta nyingine.

Katika utatuzi huo, mkuu huyo wa wilaya, anashirikiana na idara za serikali kuanzia ngazi za kitongoji, kijiji, mtaa, kata hadi wilaya na kutoa majibu moja kwa moja na wale wanaobainika kukiuka sheria na miongozo ya utumishi wa umma, wanawajibishwa.

Kwa mujibu wa Mboni, kambi hiyo itafuatiwa na ziara ya atakayofanya kijiji kwa kijiji, kata hadi kata kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi na kutatua kero zinazowakabili katika utafutaji wa haki.

**WANANCHI NAO**

Wakati huo huo wakazi wilayani hapa wameiomba serikali kuweka mkakati wa kutatua kero za wananchi badala ya kusubiri mikutano ya viongozi wa kitaifa na kisiasa kuanza kufuatilia migogoro inayoibuka katika jamii.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe, walisema hatua hiyo kuwa itasaidia kudumisha amani, ushirikiano na mshikamano baina ya wananchi na serikali na kukomesha tabia ya wananchi kujitokeza kwa wingi kutafuta haki zao wanapotembelewa na viongozi hao wa kitaifa hali inaonyesha viongozi wa chini hawawajibiki kisheria.

Walisema mikutano ya viongozi wa kitaifa imegeuka na kuwa ya kusikiliza kero za wananchi kana kwamba maeneo yao hayana viongozi.

Mkazi wa Kata ya Kagongwa, Shija William, alisema serikali inapaswa kuyafanyia kazi matatizo ya wananchi ili kuimarisha umoja na mshikamano.

Amiri Juma, Mkazi wa Kijiji cha Isagehe, alisema maendeleo na kero ni vitu viwili tofauti na kwa kutumia njia ya mikutano ya hadhara imeonyesha jinsi uwajibika wa viongozi wa umma ulivyo chini katika kutatua kero za wananchi wao.

Alisema nidhamu na maadili ni sehemu nzuri ya viongozi ya kutimiza wajibu wao na siyo kutumia lugha zisizofaa.

Ukurasa 13




Waliteketeza nyavu bila ya samaki wala elimu kwanza!

Ukurasa 12



## MIAKA 45 YA MAPINDUZI IRAN

### Yajivuna kimataifa na viasharia maendeleo. licha ya 'kigingi' cha vikwazo barabarani


# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 9, 2024 **BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA**

Nipashe


SAFARI HIFADHINI NGORONGORO KUELEKEA KIJIJINI MSOMERA

# Mchakato ulioanzia agizo la Rais, hadi mradi ujenzi unaokamilishwa na JKT

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa Handeni**

HADI sasa suala la kuhama wakazi wa Ngorongoro kupisha mahali hapo kwa hiari katika kutetea maslahi ya kimazingira, si jambo geni tena leo hii. Imepiga hatua.

Kumekuwapo mlolongo wa mazungumzo kwa nafasi ya pekee, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitumikia maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhusu Ngorongoro.

Ngazi za awali za mchakato huo wa uhamisho ulianza kupamba moto, mnamo Februari 2022, Rais Samia akawaagiza maafisa wa serikali kukutana na viongozi na wakazi wa Ngorongoro.

Serikali ikaanza kutimiza hayo ya Rais, kwa kukutana na wananchi hao wakazi wa Hifadhi ya Ngorongoro na Loliondo, kuwasikiliza na kuwaelimisha, ili kumaliza migongano iliyopo kwenye hifadhi hizo.

Akizungumza bungeni, jijini Dodoma Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akakumbusha agizo la Rais Dk. Samia akitaka viongozi wa serikali kukutana na viongozi wa maeneo ya Ngorongoro na wananchi, kurahisisha sakata hilo.

Ilikuwa hoja ya mjadala mkali na wenye tija bungeni, huku mwanazuoni Prof. Hamisi Malebo akinena mtandaoni "alichofanya Rais Samia Ngorongoro, hakijawahi kufanywa na nchi yoyote Duniani.



Kamanda wa Operesheni ya Ujenzi wa Nyumba za Kijiji cha Msomera, Kanali Mihayo, akiwa na wageni wake. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

"Nipende kusema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni wa kipekee sana, kwa sababu tulivyokuwa tukiangalia namna wananchi wa Ngorongoro walivyotendewa na tukaangalia na nchi nyingine za dunia, haipo.

"Hili ni la Tanzania pekee yake, kwanza wananchi wa Ngorongoro wamefanyiwa tathmini ya haki na uwazi ya mali zao na maboma yao wakapewa fidia. Baada ya kupewa fidia ya mali zao zote walizonazo katika maboma yale.

"Serikali ikaweka bakshishi (zawadi) kwamba anapohama, ahami bali anahamishwa, kwa gharama za serikali, anabebwa yeye, mifugo yake na mali zake zote, akishafika kule Msomera ambako awamu ya kwanza waliojiandikisha kwa hiari walipelekwa anapewa nyumba.

"Ile nyumba sio sehemu ya fidia ni zawadi, na nyumba ipo kwenye eneo la ekari mbili na anapewa na hati bure bila gharama yoyote bila kutoa hata shilingi moja."

Hiyo inaendana na kubukumbu ya taarifa zilizotolewa Julai 2022, kwamba zipo shilingi bilioni 700 za kuwahamisha wakazi wa Ngorongoro, jumla ya kaya 22,000, ikiwa ni hatua ya kupisha ustawi wa ikolojia ya kwenye eneo hilo.

**TAARIFA KUHAMA**

Mnamo Oktoba mwaka jana, ikatolewa taarifa ya kiserikali, kaya 11 na wananchi 43 pamoja na mifugo 36 walioamua kuhama kwa hiari kupisha uhifadhi Oktoba19, 2023 wanampongeza Rais Dk.Samia, kwamba ni hatua inayoboresha maisha yao na vizazi vyao.

Wakazi hao wakaenda kuhamia katika maeneo waliyoyachagua wenyewe kwa hiari katika; wilaya za Monduli, Meatu, Arusha vijijini, Simanjiro na Handeni.

Pia, taarifa ya utekelezaji mradi huo wa Uhamisha Watu Awamu ya Pili, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Mdala Fedes, akabainisha serikali imeongeza idadi ya nyumba zinazojengwa kutoka 503 za awamu ya kwanza hadi kufikia nyumba 5,000 katika awamu ya pili.

Pia, ikasogeza huduma za kijamii kama vile maji, shule, vituo vya afya, umeme, barabara, mawasiliano na huduma za mifugo na posta.

Mradi wa ujenzi wa nyumba sasa umepanuka katika maeneo mengine ya mkoa wa Manyara na wilaya za Kilindi na Handeni, nyumba 1500 zilikuwa zinatarajiwa kujengwa katika kijiji cha Kitwai B wilayani Simanjiro; 1,000 kijiji cha Saunyi, Kilindi; na nyumba zingine 2500 kijijini Msomera,

**INAENDELEA UK.14**

UCHUMI

MIAKA 45 YA MAPINDUZI IRAN

# Yajivuna kimataifa na viashiria maendeleo licha ya 'kigingi' cha vikwazo barabarani

- Watalii mil. 5; magari yao; wataalam ndani 100%; mabwawa umeme 660...
- Yakana kuwapo viashiria vya marufuku za kidini

**Na Mwandishi Wetu**

Februari 11, 1979 ni siku ya historia kwa watu wa Iran, ambayo Imam Khomein aliongoza mapinduzi yaliyoung'oa utawala wa kiongozi Shah na kuwa hatua ya kuzaliwa Jamhuri ya Kiislam ya Iran.

Miaka 45 imetimia sasa, baada ya mapinduzi hayo, kwa mtazamo wa baadhi ya watu Iran imejengewa dhana ya nchi ya Waislam wa misimamo mikali au siasa kali, nchi ambayo asiye Muislam, hana uhuru wa kuabudu.

Dk. Mohsen Maarefi, ni Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni katika Ubalozi wa Iran nchini Tanzania, anaanzisha ufafanuzi wake, akipinga hilo halina ukweli, badala yake anasisitiza wasio Waislam wana haki ya kuabudu, kama ilivyo kwa Waislam.

Anakiri Iran ni nchi ya Kiislam na zaidi ya asilimia 90 ya wananchi wake ni wa Imani hiyo, lakini anatoa anangalizo kwamba haina maana kwamba watu hawana nafasi na haki ya kuendesha shughuli zao kidini.

Dk. Mohsen anazitaja baadhi ya imani za dini nyingine zilizopo Iran, kuwa ni Ukristo na imani ya dini ya Bahai, Zorostriani, imani za kiyahudi na nyinginezo.

Anasema waumini wa dini hizo uwapo wao unatambulika kisheria, pia wana haki ya kufanya ibada zao na wana sehemu maalum za kufanyia ibada.



Gari aina ya Dena, inayozalishwa kwa teknolojia ya ndani, nchini Iran. **PICHA ZOTE: MATKTABA.**

**ULINGO WA UCHUMI**

Akizungumzia maendeleo ya kiuchumi ya Iran kwa miaka 45 baada ya mapinduzi, Dk Mohsen anasema Iran imepiga hatua kubwa, licha ya vikwazo vya kimataifa vya kiuchumi, inavyowekewa.

Moja ya maeneo ambayo nchi ya Iran imepiga hatua ni kwenye usafiri wa anga, Shirika la Ndege la Iran maarufu Iran Air au Huma, analitaja kupiga hatua kubwa na kwa sasa linarusha ndege zake katika maeneo 72 tofauti nje ya Iran.

Pia, Iran inatajwa ipo vizuri kwa usafiri wa barabara, maeneo yote ya miji mikubwa na midogo yanafikika kwa usafiri wa barabara zenye lami.

Jambo la kujivunia kwa mujibu wa Dk Mohsen ni kwamba barabara hizo zimejengwa na wahandisi wa ndani waliosoma na wanafanya kazi nchini humo.

Dk. Mohsen, pia anasema kwamba hata madaraja makubwa na madogo katika miji yote nchini Iran, yamejengwa na wahandisi wa Iran hakuna ajira kutoka nje.

**UTALII WA IRAN**

Iran ni nchi inayosifika duniani kwa kuuza mafuta na gesi, pia ikitumia vyema utalii wake kuboresha uchumi wake, ingawa sekta hiyo imekuwa ikikumbana na vikwazo mbalimbali, kuanzia vita ya Iran na Irak iliyodumu miaka minane, 1980 hadi 1988 pamoja na vikwazo vya kiuchumi kimataifa.

Mnamo Mwaka 2014-15, baada ya kuondolewa kwa vikwazo dhidi ya Iran, mkurugenzi huyo anataja sekta ya utalii ilikuwa kwa kiwango cha kuvutia, zaidi ya watalii milioni tano waliitembelea Iran.

Anasema hadi mwaka 2019, sekta ya utalii ilikuwa kwa kiwango cha kuvutia, idadi ya watalii ilifikia milioni tisa, ingawa hali ilianza kuwa mbaya na idadi ya watalii kupungua, baada ya janga la maradhi ya corona.

Hata hivyo, Dk. Mohsen anafafanua, baada ya shida janga la corona kupatiwa suluhisho, sekta ya utalii, ikaanza kukua kwa mara nyingine na hadi mwezi Septemba na Oktoba 2023, idadi ya watalii nchini Iran ilifikia milioni 5.2.

Iran pia, sasa inafanya kazi kubwa ya kuhamasisha utalii wa ndani, ikiwa ni kati ya nchi za mfano duniani, kwa mwaka 2021 takwimu zinaonyesha kuwa watalii wa ndani walitumia kiasi cha Dola za Marekani bilioni 33.3.

Malengo ya taifa hilo ni kuiboresha sekta ya utalii kwa kuongeza uwekezaji na kuhakikisha idadi ya watalii inafikia milioni 20 itakapofika mwaka 2025.

Moja ya maeneo Iran imeendelea kujivunia na kujipatia umaarufu katika utalii ni kisiwa cha Kish, kinachotajwa ni kati ya visiwa 10 duniani vinavyovutia zaidi na kwa mwaka, mamilioni ya watu kutoka sehemu mbalimbali duniani hukitembelea.

Inaelezwa, watalii wengi wanaotembelea Iran ni kutoka nchi za Asia na wengine asilimia 10 wanatoka zaidi nchi za Umoja wa Ulaya na Marekani.

**HAKI YA MWANAMKE**

Haki ya mwanamke Iran, imekuwa ikitajwa kuwa ni nchi ambayo wanawake wapo nyuma, mamlaka haziwapi nafasi.

Dk. Mohsen anapingana na hoja hiyo na kukumbusha kwamba nafasi ya mwanamke wa Iran ina historia ndefu akinena "tangu wakati wa mapambano ya kuung'oa Utawala wa Shah."

Anafafanua kuwa, wanawake walitumika kuhamasisha wanaume kushiriki mapambano, kuhudumia majeruhi waliotokana na maandamano na migomo dhidi ya utawala, pia baadhi yao walishiriki katika migomo na maandamano hayo.

Anarejea rekodi kwamba, wapo baadhi ya wanawake walioteswa, kukamatawa na wengine kuuawa wakati mapinduzi yalipopamba moto.

Kwa mujibu wa Dk Mohsen, wanawake wa Iran sasa wamepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali na wengine wamekuwa maarufu duniani kwa heshima wanazopata kimataifa.

Anamtaja Mariam Mirzakhani, mwanamke aliyezaliwa na kukulia Iran, aliyeonyesha uwezo wa hali ya juu katika somo la hesabu hadi kwenda kusoma Chuo Kikuu cha Stanford nchini Uingereza.

Mariam ambaye alifikia hatua ya kuwa Profesa wa Hesabu katika chuo hicho, mwaka 2014 alitwaa tuzo (Fields Medals) na kuwa mwanamke wa kwanza kutwaa tuzo hiyo na mwanamke wa kwanza kutoka Iran kutwaa tuzo hiyo.

Zaidi ya hilo, Dk. Mohsen anasema, wanawake wa Iran wamepata mafanikio makubwa kwenye michezo mbalimbali ambayo wamekuwa wakishiriki, ikiwamo soka.

Anawasisistiza kwamba, kiloichoko sasa wanawake Iran hakop mbele na wanaodhani wako nyuma 'wajaribu kuutafuta ukwel'i na wataona uhalisia; 'wamekuwa mstari wa mbele katika kila sekta nchini humo.'

**VIKWAZO UCHUMI**

Akizungumzia vikwazo vya kiuchumi, ambavyo nchi hiyo imekuwa ikiwekewa, Dk Mohsen anasema anakiri ukweli huo, lakini Iran imeendelea kupiga hatua zake kwa kuwa sio nchi tegemezi.

Anatoa mfano wa kampuni ya magari ya Iran ambayo ni bora na yamekuwa yakiuzwa katika nchi Jirani, akitoa mfano Irak na kwa sasa wameanza kuuza magari hayo nchini Senegal.



Dk. Mohsen Maarefi, ni Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni katika Ubalozi wa Iran nchini Tanzania.

"Pamoja na vikwazo vya kiuchumi, Iran kwa sasa tunazalisha magari yetu, ukiona gari aina ya Dena jua hilo ni kutoka Iran. Ni magari bora, hata mimi nikiwa Iran, ndiyo aina ya gari ninayotumia," anasema Dk Mohsen.

"Hivi ninavyozungumza Iran inashika nafasi ya 10 duniani kwa kutengeneza magari mengi kila mwaka, ikiwa imeizidi nchi za Ufaransa, Italia na Uingereza.

Akifafanua zaidi kuhusu maendeleo anasema nchini Iran kwa sasa umeme upo hadi vijijini, pamoja na huduma nyingine kuanzia maji, gesi hadi huduma za intaneti.

Dk. Mohsen anafafanua kuhusu umeme, kwamba, kabla ya mapinduzi, Iran ilikuwa na mabwawa 19 ya kuzalisha umeme, lakini sasa yamefikia 660 ambapo nchi hiyo inazalisha umeme na kuuza kwa majirani zake.

**MIRADI YA NYUKLIA**

Akizungumzia matumizi ya nyuklia, ni kwamba nchi hiyo imekuwa ikituhumiwa kuwa na lengo la kujiimarisha kijeshi, Dk. Mohsen anasema Iran wanatumia nishati hiyo kwa maendeleo ya viwanda, si kwa ajili ya vita kama inavyotangazwa duniani.

"Kiongozi wa juu nchini humo, Ayatollah Khamenei alishapitisha amri (hukumu-fatwa) kupiga marufuku matumizi ya nyuklia katika vita kwa sababu mabomu ya nyuklia yanaharibu kila kitu si adui tu bali yanaharibu mazingira, viumbe, mimea na hata watu wasio na hatia," anasema Dk Mohsen.

**MIRADI MAENDELEO**

Eneo jingine ambalo Dk. Mohsen anasema nchi yake imepiga hatua ni kwenye tiba ya uzazi ambapo watu wenye matatizo ya uzazi wamekuwa wakifanyiwa tiba kwa gharama nafuu nchini Iran na kufanikiwa.

Kwa mujibu wa Dk Mohsen watu wa mataifa mbalimbali wamekuwa wakifanya utalii wa tiba nchini Iran kutokana na maendeleo ya nchi hiyo katika sekta ya afya.

"Rekodi zilizopo ni kwamba watu zaidi ya milioni 1.2 wamefanya utalii wa tiba na afya nchini Iran na kunufaika na maendeleo ambayo nchi hiyo imepiga katika sekta ya afya," anasema Dk. Mohsen.

Anasema kwamba kwa sasa wapo katika mpango maalum kuhakikisha kwamba kwa siku zijazo kila Mtanzania anayetaka kwenda kutalii Iran atakuwa huru kufanya hivyo bila kutumia viza.

"Watanzania watapata nafasi ya kutumia fursa hiyo kuingia katika nchi ambayo pia inasifika kwa amani," anasema.



TAFAKURI YA MLALAHOI

## Waliteketeza nyavu bila ya samaki wala elimu kwanza!






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

"UCHOMAJI nyavu haramu za uvuvi, unarudisha nyuma maendeleo ya uvuvi, pia inaongeza chuki ya wavuvi kwa serikali wizara ongezeni kasi ya kuwapa elimu wavuvi wetu."

Hiyo ni kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa viongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Januari 30 mwaka huu jijini Mwanza, akizindua vizimba vya kufuga samaki na kutoa boti kwa wavuvi.

Bila shaka, kauli hii ya mkuu wa nchi, inafikirisha sana. Inaoneysha Chifu Hangaya ana akili kubwa. Wao walikuwa wanaona ni bora akipatikana mvuvi haramu, adhabu iwe kuporwa zana.

Lakini si tu kuporwa zana, bali zana hizo pia ziteketezwe iwe kwa kuchomwa moto au kupondwapondwa, kama si kumwagiwa tindikali, ili mradi ipotee machoni mwetu.

Kauli hiyo inaweza kuwashangaza wengi, kwa sababu walishazoea kwamba nyavu zinachomwa moto, huku ukimwona mzito wa wizara ndiye anaongoza kwa kushika mwenge wa moto, baada ya kuzimwagia petroli na kuziwasha.

Hapo hufuatiwa na makofi na hata kama wananchi hawana hisia za kupiga makofi, utamsikia 'emsii' akihimiza piga makofiii! na wananchi kuyapiga

wa, wa, waaa! Inakuwa ni sherehe, lakini huku wenye nyavu zao wakiugulia.

Tulishazoea haya mambo na kuyakubali, tukishashuhudia nyavu kuchomwa moto na kama kuna mitumbwi imekamatwa, basi kama si kutaifishwa, basi nayo iteketezwe, kukomesha uvuvi haramu unaotumalizia samaki.

Ni kweli, kuvua samaki vifaranga ni hatari kwamba tunapunguza kizazi cha samaki na kutoishia kutoweka maziwani, baharini na mitoni na hatimaye kukosa chakula, pia kuathiri uchumi wa taifa.

Lakini je, kuchoma nyavu ndiko kunaongeza samaki? Je, anayechomewa nyavu zake, baada ya hapo huishi vipi kama si naye kuteketea kimaisha?

Bila shaka Chifu Hangaya kaliona hilo. Yeye anaamini, kwamba kwa kutoa elimu ya madhara na ubaya wa uvuvi

haramu, wananchi wana uwezo wa kuelewa na kama watasaidiwa na kuwezeshwa, bila shaka wataelewa umuhimu wa uvuvi halali na kuachana na haramu.

Wakati mwingine, huwa najiuliza hivi nyavu hizo zinapokamatwa, huwa hazikutwi na samaki wasiotakiwa kuvuliwa? Mbona sijashuhudia samaki hao wakiteketezwa sambamba na nyavu zao? Pengine huteketezewa matumboni.

Mnakumbuka mwaka 2009, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, John Magufuli, alikamata samaki waliovuliwa kwa njia haramu na wavuvi kutoka Vietnam? Hakukamata nyavu, bali samaki, ambao hatimaye tuliwafaidi sisi wenyewe Watanznaia kwa kuwala.

Tatizo la nchi hii, kauli kama hii ya Rais hudumu muda mfupi tu na baadaye tunajisahaulisha na kurejea tulikotoka na hasa pale rais anapooondoka na kuja mpya.

Jasiri wangu ni Chifu Bagolole, katika ziara yake ya 'Back2Back' nimemshuhudia akihimiza watu kuonyesha mabango yenye kero, katika mikutano yake Kigoma.

Akikemea wanaozuia watu kuonyesha mabango hayo, kwani ndiyo njia mwafaka ya kufikisha ujumbe wenye kero zao kwa CCM na yeye kama kiongozi wa chama hicho, kuzitafutia ufumbuzi sawia.

Siku hiyo nilimkumbuka Chifu Chalamila alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, aliyehamasisha watu kufika na mabango kwenye mkutano wa Chifu Hangaya. Ila siku chache baadaye alifungasha virago vyake.

Ilitokea hivyo, lakini akajikuta anafungasha virago, akiwa mwakilishi wa mamlaka ya juu kitaifa. Ilikuwa ishara tosha kwake kwamba, hakuwa na uwakilishi bora wa dola kuu kitaifa, ilimtokea yeye na baadhi ya wenzake wenye cheo kama chake.

Suala la Chfu Hangaya kukemea, linataka kutuonyesha kuwa hakuna sehemu salama nchini katika suala la uongozi, kwamba wawakilishi wengi hawamudu vilivyo kazi zao.

Kutokana na hilo, tafsiri yake inajionyesha katika kuchukua hatua ya kuteketeza nyavu zinazodaiwa kuwa haramu badala ya kutoa elimu, pia kuibuka mabango, badala ya kero kutatuliwa bila ya kumsubiri, kiongozi wa kitaifa afike kusikiliza kero.

Tatizo lililopo kwa baadhi ya viongozi wetu ni kutojiamini, kwamba wakichukua hatua wataharibu na kumkasirisha mteuzi, au pengine wakichukua hatua mteuzi akifika atakosa la kuwaambia wananchi kuhusu kero, matokeo yake kumbe wanalimbikiza kero na serikali kugeuka adui wa watu wake.

Kwa hali ilivyo ya kiongozi mitaani, wilayani na hata mikoani, ipo haja ya kufanyika tathmini ya kina gani tupate viongozi wa kuwakilisha wananchi, iwe kwa kuteuliwa au kuchaguliwa na wanaoongozwa, ili wawadhibiti wenyewe huko waliko, ziara iendelee.



Makazi mapya kijijini Msomera, Handeni shughuli za ujenzi na nyumba mpya zilivyo. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

# Mchakato ulioanzia agizo la Rais, hadi mradi ujenzi unaokamilishwa na JKT

**INATOKA UK. 11**

wilayani Handeni,

**JKT WATEKELEZA**

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ndilo lililopewa mradi huo wa nyumba 5,000 za wanaohama kutoka Ngorongoro kwa hiari, nyumba zikijengwa katika wilaya tatu.

Kijiji hicho ambacho kina muonekano wa mpangilio wa ujenzi wa nyumba hizo,tayari kuna wakazi wa awamu ya kwanza tayari wameanza maisha yao ikiwemo kuendesha shughuli zao za kilimo na ufugaji katika maeneo yao.

Nyumba hizo ambazo zimependezesha kijiji hicho, zina wakazi ambao wameanza maisha ikiwemo kufanya biashara mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii ua hapo.

Jeshi hilo limekipendezesha kijiji hicho kutokana na ubora wa nyumba uliopo ikiwemo kuwajengea majosho kwa ajili ya kuosha mifugo, pamoja na mashamba.

Hii ni awamu ya pili ya wananchi walioamua kuhama kwa hiari kutoka katika hifadhi hiyo na kuja kuanzisha makazi mapya ambapo kila familia inakabidhiwa nyumba.

Katika awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 5,000

kuanzisha makazi mapya, 2,500 zitajengwa 1,000 katika kijiji cha Sainyu na 1500 katika kijiji cha Kitwai B,wilayani Simanjiro.

Ujenzi huo ulianza Oktoba mwaka jana, mpaka sasa nyumba zilizokamilika ni 1,000 na nyingine ziko katika hatua nzuri za ukamilishaji Mamlaka ya Maliasili, kwa kushirikiana na wilaya ya Handeni ndio wanaoratibu kazi hiyo, kaya 64 tayari ziko mbioni kukabidhiwa nyumba hizo za makazi mapya.

**NENO LA WAJENZI**

Msimamizi wa mradi huo, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, anasema kijiji hicho kitakuwa na huduma bora kama walizozipata wakazi wakiwa Hifadhi ya Ngorongoro, tena zikiboreshwa maradufu na serikali inajipanga kuhakikisha huduma stahiki zinapatikana.

Brigedia Jenerali Mabena anasema, awali watu hao hawakuwa ahadi walizopewa, lakini baada ya kuhamia makazio mapya wameshuhudia na sasa wanaendelea kuwashawishi wenzao wahame walikokuwa.

"Nashukuru watu wameelewa nyumba walizozikuta, hivi sasa wanazidi kuja kuhamia," anasema Brigedia Jenerali Mabena.

Anafafanua kuwa JKT iko katika hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa nyumba za wakazi hao, kazo inayofanywa na Shirika la Uchumi JKT- Suma JKT.

Anasema kuwa nyumba hizo kwa mujibu wa maelekezo kutoka kwa Rais Dk. Samia, ni zenye vyumba vitatu kwa ajili ya watoto wa kike na kiume na wazazi, akisifu wakazi waliohamia katika eneo hilo, wengi wanafurahia na kuipongeza JKT kwa kazi yake.

Kamanda mwingime wa mradi, Kanali Sadick Mihayo, anataka mbali na kijijini Msomela, akisema nyumba hizo zina maeneo makubwa ekari mbili na nusu, zinazomuwezesha mkazi kufanya chochote cha kumuingizia kipato na familia yake.

Anajisifu JKT haijawahi kufeli katika kazi yoyote wanayokabidhiwa, hivyo anaihakikishia serikali ujenzi huo unakamilika kwa wakati.

**WAKAZI MSOMERA**

Flora Utumo, kutoka Ngorongoro, anasifu maisha mapya ni mazuri, kwa sababu wamepewa uwanja mkubwa na nyumba, jambo ambalo walikotoka halikuwapo, kutokana

na ufinyu wa maeneo.

Anasema kuna huduma za shule, hospitali vyote vinapatikana kijijini Msomera, akiisifu serikali kuiwatendea jambo jema wakazi wa Hifadhi ya Ngorongoro.

"Kwenye hifadhi kulikuwa na ugumu wa kufanya shughuli za kibinadamu za kuwapatia chakula, lakini hapa Msomera vyote vinapatikana na tumepewa eneo la ekari mbili na nusu," anasema Flora, akitaja pia wanapewa ardhi ekari tano kwa ajili ya kuendesha kilimo chao cha kila siku

Kwa upande wake, mkazi Sailep Melea, anasema tofauti ya Ngorongoro na Msomera, ni kwamba makazi mapya yana hati miliki ya maeneo wanayoyamiliki.

Pia, anasifu tayari shule imejengwa inaitwa Samia Suluhu Hassan, wanafunzi wengi wapo na wanaendelea na masomo kama ilivyo kawaida.

Mwanafunzi Lydia Lekrimi, anasifu shule anayosoma ni nzuri na kunaa walimu kama ilivyokuwa awali Ngorongoro.

Anaisifu shule ya Msomela iko karibu sana na

Nyumbani wanakoishi, hivyo safari ya shule haiwachoshi kama ilivyokuwa Ngorongoro, huku darasani wanafunzwa vizuri, nao mahudhurio yao ni mazuri.

**MWENYEKITI KIJIJI**

Martine Olakayo, anaipongeza serikali kutokana na kufanya mambo mazuri katika kijiji hicho, kwa sababu awali hawakutegemea watu waliohamia watakinogesha kijiji hicho.

Anasema tayari kijiji chao, serikali imewawekea miundombinu ya kutosha kama barabara, maji, shule, hospitali na mahitaji mengi ya kibinadamu.

Vilevile anautaja mradi wa kibiashara, wamejengewa kituo cha kukusanyia maziwa, ambakohawana shida yoyote kwenye soko la maziwa, sasa anopga yote walibaki Ngoropngorol wafike Msomera.

**DC HANDENI**

Albert Msando ni Mkuu wa Wilaya ya Handeni, anayesema waliohamia kwao, wasirubuniwe, wafike kumiliki ardhi kijijini Msomera na vingine ambavyo wanakwenda kuhamia, hakuna cha mahitaji yao kitakachokosekana.

Msando anasema, serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba hizo za wageni wanaohamia na anawataka wafanyabiashara wakazi wawape ushirikiano wateja wapya kutoka Ngorongoro, akitoa tahadhari mkwa atakayethubutu kuwarubuni wateja hao wapya.





# Mfumo ufundishaji mubashara wazinduliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MFUMO wa ufundishaji mubashara kwa wanafunzi wa sekondari umezinduliwa, ambapo mwalimu mmoja anaweza kufundishisha shule zaidi ya moja kwa wakati mmoja.

Hatua hiyo ni mojawapo ya mkakati wa serikali kupunguza uhaba wa walimu katika maeneo mbalimbali, kwa sasa imefikia 271,028.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa akizindua majaribio ya ufundishaji wa mfumo huo juzi mkoani hapa kati ya Shule ya Sekondari Dodoma na Shule ya Sekondari Kibaha mkoani Pwani alisema hatua hiyo ni moja ya jitihada za serikali ya kupunguza uhaba wa walimu nchini na kuongeza maarifa kwa wanafunzi.

"Nilitoa agizo la kutaka ufanyike msawazo wa walimu bado kumekuwapo na uhaba wa walimu katika ngazi zote za elimu ya awali, msingi na sekondari, mpaka muda huu nimesimama hapa nazungumza uhaba ni walimu 271,028 ambao walipaswa kuwa kwenye shule zetu na ndiyo maana tumekuja na teknolojia hii ya elimu mubashara,"alisema.

Alibainisha kuwa kwa upande wa elimu ya awali na msingi uhaba ni walimu 186,385 na kwa sekondari ni 84,643.

"Tunakwenda kwenye majaribio ya TEHAMA ya ufundishaji mubashara, tunatambua kutakuwa na changamoto mbalimbali na changamoto ya kwanza ni uhaba wa vifaa, niwaelekeze wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha wanatenga kwenye bajeti ijayo ya 2024/25 fedha za kutosha ili tuanze mchakato wa kununua vifaa hivi vya TEHAMA," alisema.

Kadhalika aliwaelekeza wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kuteua shule maalumu ambayo itakuwa nguzo ya kusambaza mifumo huo wa TEHAMA katika shule mbalimbali katika maeneo yao.

"Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknlojia nawaagiza kwenda kutekeleza programu hii ili isambae nchi nzima," alisema.

Aliongeza kuwa: "Mpango wa TAMISEMI ni kuhakikisha ifikapo Desemba 2025 ufundishaji mubashara uwe umeenea nchi nzima, ili kusaidia vijana wetu kupata elimu iliyo sawa hivyo endeleeni kufanya mapinduzi makubwa ya TEHAMA ambayo yataleta usawa na tija kwa wanafunzi wote wanaosoma elimu ya awali, msingi na sekondari".

Pamoja na hayo, Waziri Mchengerwa alisema TAMISEMI wanakwenda kutekeleza suala la msawazo wa walimu shuleni na inakuja na mkakati ya kuwafanya walimu waliohitimu shahada au stashahada ya ualimu kufundisha katika shule za serikali kwa muda wa miezi sita au mwaka mmoja kwenye shule mbalimbali hasa kwenye maeneo wanayotoka. Mwalimu wa Shule ya Sekondari Dodoma, Laurian Nyoni, alisema mfumo huo utasaidia katika ufundishaji hasa kutokana na kuwa walimu kuhitaji zana za kufundishia na unaongeza hamasa kwa wanafunzi kujifunza.



Waziri wa Kilimo, Husssen Bashe (wa tatu kushoto) na Mkurugenzi wa Mawasiliano na Masoko wa kampuni ya GF Automobile, Salman Karmali (wa pili kulia) wakikata utepe jijini Dodoma jana, wakati wa hafla ya kukabidhi gari iliyotolewa na kampuni hiyo, kwa ajili ya mradi wa Kilimo BBT, wakiwa na lengo ya kuunga mkono serikali katika sekta ya kilimo. **PICHA: MPIGAPICHA WET**U

# Watoto waliofungiwa, kupewa mafunzo ya dini warudishwa nyumbani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MABINTI 132 waliokutwa wamefungiwa katika nyumba moja jijini hapa wakipatiwa mafunzo ya dini ya kiislamu na Kituo cha Al- Habash wamekabidhiwa kwa wakuu wa wilaya walizotoka ili kurudishwa katika familia zao.

Aidha kati yao mabinti hao, 14 wamebainika kuwa walikatishwa masomo, hali iliyomlazimu Mkuu wa Mkoa wa Dododoma, Rosemary Senyamule kuwaagiza wakuu wa wilaya katika maeneo walikotoa kuhakikisha wanarejeshwa shuleni.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Senyamule alisema ripoti ya awali ya ufuatiliaji wa sakata hilo imebaini kuwa wapo baadhi waliokatishwa masomo.

"Ripoti ya mabinti hao imebaini kuwa wapo baadhi yao waliokatisha masomo na wengine waliobadilishwa majina pia kituo hakikuwa na leseni ya usajili wowote wa kutoa huduma hiyo" alisema Senyamule.

Kufuatia majibu ya ripoti hiyo, Senyamule aliielekeza watoto 132, wakabidhiwe kwa wakuu wa wilaya katika maeneo wanayotokea, kisha kurejea shuleni huku hatua za kisheria zikiendela kuchukua mkondo wake.

Senyamule, alisema kati ya watoto hao wapo 14 ambao ni wanafunzi waliokatishwa masomo na kujiunga na kituo hicho ambacho kilikuwa kikifundisha dini ya kiislamu. "Maagizo ya serikaili kuwa watoto wote warejeshwe kwenye maeneo yao walikotoka kwani uchunguzi umebaini kuwa kati ya watoto wote, 14 walikuwa wanafunzi ambapo wanne walihitimu darasa la saba mwaka jana na walikuwa hawajajiunga na kidato cha kwanza licha ya kufaulu lakini pia 10 walikuwa ni wanafunzi wa kidato cha pili" alisema Senyamule.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri alisema kati ya mabinti hao waliokutwa katika kituo hicho, 62 wana umri wa zaidi ya miaka 18.

"Sasa hawa wa miaka hii wao wanaouwezo wa kupima maisha waliyokutana nayo hapa na kufanya uamuzi lakini kwa wengine ni shida ndiyo maana kamati ya ulinzi na usalama iliamua kuwachukua na kuwatoa katika kituo hichi na kuwapeleka kwenye kituo cha makao ya watoto" alisema.

Februari 2, mwaka huu Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Dodoma ilipata taarifa za uwepo wa kituo hicho na kubaini hakina usajili ambapo Februari 3, ilitoa maagizo ya kufungwa.

# Tume ya Kurekebisha Sheria yawaita wadau kutoa maoni

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imewataka wadau wa sheria nchini kuwasilisha maoni yao juu ya sheria mbalimbali kupitia tume hiyo ili ziweze kufanyiwa kazi kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, George Mandepo alisema hayo jana mkoani hapa wakati wa kufanyia tathmini ya maoni yaliyotolewa na baadhi ya wananchi kwenye maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyohitimishwa Februari Mosi, 2024.

Wakati wa maadhimisho hayo ambayo yalifungwa na Rais Samia Suluhu Hassan wananchi wengi waliomba Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kuwatembelea maeneo yao ili kupata maoni yao kuhusu utekelezaji wa sheria mbalimbali hapa nchini.

Mandepo alisema tume hiyo imekuwa ikikutana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku na wakati wa kufanya utafiti na utoaji wa elimu ya sheria kwa umma.

"Mwananchi mmoja mmoja au vikundi wamekuwa wakipata fursa ya kutoa maoni yao kwa njia mbalimbali ikiwemo kupitia barua pepe, barua ya kawaida, kupiga simu au kuonana moja kwa moja na maofisa husika wa tume ili kueleza changamoto wanazoziona katika sheria zilizopo au upungufu wowote kwenye utendaji ambayo wanadhani yanahitaji kuwekewa mfumo wa sheria," alisema.

Aliongeza kuwa tume hiyo pia imekuwa ikikutana na wananchi wakati wa utafiti kutoa elimu kwa umma na wakati wa tathmini lakini bado wananchi wanaweza kuandika, kupigia simu au kutembelea ofisi za tume, kutoa maoni yao ambayo yatapokelewa na kuyafanyia kazi kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

Aidha akitolea ufafanuzi swali lililoulizwa na mwananchi aliyeomba tume iwe inatembelea mahabusu na ikiwezekana wanasheria wakakae magerezani kama wafungwa ili waweze kuviona vipengele vya sheria vinavyostahili kufanyiwa marekebisho.

Mandepo alisema idara ya magereza ni moja ya mdau muhimu wa tume pia ni eneo mojawapo la kupata taarifa za kitafiti zitakazosaidia pia kufanya marekebisho ya sheria kama ilivyowahi kupendekezwa na Tume ya Haki Jinai.





## Makete 'yajifunga mkanda' ukamilishaji miradi ya maji

**Na Elizabeth John,** MAKETE

SERIKALI wilayani Makete Mkoa wa Njombe imesema itahakikisha inakamilisha miradi yote ya maji wilayani hapa, ili wananchi wapate huduma hiyo kwa uhakika.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda wakati anakagua mradi wa maji wa Usalimwani-Mfumbi-Ruaha utakaonufaisha wananchi 4,124 wa wilaya hiyo.

"Mradi huu kama mnavyojua ni muhimu sana, bado kuna mahitaji makubwa ya maji lakini sambamba na hapo kiujumla ukiacha eneo hili kwa sababu tunategemea maji yakishatoka katika Kata ya Mfumbi, Kitulo na Ipelele tutakuwa tumefika asilimia 100 kwa sasa tuna asilimia 90 ya upatikanaji wa maji," alisema Sweda.

Alisema kuwa Wilaya ya Makete gharama za utekelezaji wa miradi ya maji siyo kubwa kwa sababu wanategeea kwenye milima na kuyashusha kwenye matangi na kwenda kusambazwa kwa watu kwa njia ya mseleleko.

Hata hivyo alisema tayari wilaya hiyo imetengeneza mpango wa maji na usafi wa mazingira.

"Sehemu nyingine haipo na wataalamu walishamaliza kukamilisha hilo andiko, tumetembea katika kata zote na kwenye mpango wetu tunajua sasa tunazaidi ya vyanzo vya maji 800," alisema Sweda.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Innocent Lyamuya alisema kazi zilizotekelezwa mpaka sasa ni uchimbaji wa mtaro ya njia kuu ya maji, ununuzi wa bomba, ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji na ununuzi wa pikipiki moja.

Lyamuya alisema mradi huo unatekelezwa kwa miezi nane na mkandarasi M/S HARFRE TECH kwa Sh.milioni 736.7.

"Kuna changamoto kidogo ya malipo mkandarasi aliomba malipo ya awali lakini yalichelewa, vile vile kwa kazi waliyoifanya mtaro peke yake zaidi ya Sh. milioni 150 kwa hiyo anaupungufu wa fedha," alisema Lyamuya.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Mfumbi, Eveline Mpande aliishukuru serikali kwa kuanza mradi huo ambao utasaidia kuwaondoa katika adha ya kutembea umbali mrefu kufuata maji safi na salama.



Katibu wa NEC ya CCM Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda akizungumza na wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya juzi, akiwa katika ziara ya kusikiliza kero za wananchi katika mikoa mbalimbali nchini. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Madiwani wasusia kikao kisa sheria kuchakachuliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wamesusia kikao cha baraza wakipinga kitendo cha serikali kuchakachua sheria ndogo waliyoitunga ya kusimamia ukusanyaji wa ushuru wa mazao ndani ya halmashauri hiyo.

Wananchi hao wamesema mabadiliko hayo yanalenga kuwaumiza wakulima.

Tukio la madiwani hao kususia kikao lilitokea jana baada ya kusomewa taarifa ya kamati ya fedha ambayo ilionyesha kuwa mchakato wa kutunga sheria hiyo ya kusimamia ushuru wa mazao umekamilika na sasa iko tayari kwa matumizi.

Diwani wa Kata ya Lujewa, Jeremiah Makao ndiye aliyeanza kuhoji kuhusu kifungu hicho ambacho kilionekana kimerekebishwa tofauti na namna madiwani walivyokipitisha wakati wakitunga sheria hiyo.

Makao alisema kuwa katika sheria waliyoitunga ilielekeza ushuru utozwe kwa mtu anayesafirisha kutoka kata moja kwenda nyingine au nje ya Wilaya ya Mbarali ndiye atapaswa kulipa ushuru.

Alisema katika sheria iliyokamilika na tayari kwa kutumika inaonyesha kifungu hicho kimebadilishwa na kinaelekeza kuwa mtu yoyote anayesafirisha mazao kutoka mahali popote ndani ya halmashauri hiyo atapaswa kulipa ushuru.

Diwani Makao alisema kuwa kifungu hicho kinakwenda kuwagombanisha na wakulima ambao tangu zamani walikuwa wakitozwa ushuru wakati wakisafirisha mazao yao kutoka shambani kwenda nyumbani na kwamba waliwaahidi kutunga sheria ya kutatua jambo hilo, lakini inaonekana sheria hiyo haijaondoa kero hiyo.

"Tulikuwa tunakusanya ushuru wa mazao kwa taabu tukigombana na wananchi wetu, na sisi madiwani tukawaahidi kurekebisha sheria ili kuondoa kero hiyo na tukusanye ushuru kwa hiyari kutoka kwa wananchi bila kuathiri mapato ya halmashauri, sasa kifungu hiki kuachwa hivi tutakuwa hatujaondoa kero ya wananchi wetu," alisema Diwani Makao.

Diwani wa Kata ya Imariro Usongwe, Chuki Jeremiah akahoji mamlaka ya kubadilisha sheria iliyotungwa na Baraza la Madiwani kwa mujibu wa sheria yametoka wapi na ikiwa mamlaka hayo uapo kwa mtu au mamlaka nyingine ya kiserikali basi hakuna sababu ya uwepo wa baraza hilo.

Akijibu hoja hizo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbarali, Misanna Kwangula alisema mchakato wa kutunga sheria ndogo huanzia kwenye baraza la halmashauri ambalo ndilo lenye mamlaka kisheria ya kutunga sheria ndogo.

Alisema baada ya baraza kumaliza kazi yake, mapendekezo ya sheria hiyo hupelekwa kwenye ofisi ya mkuu wa mkoa ambako pia wataalam wanaipitia na kisha kumpelekea waziri mwenye dhamana.

Alisema waziri mwenye dhamana naye anao wataalam wake ambao pia huipitia kabla ya kuirejesha kwenye halmashauri kwa ajili ya kutumika.

Alisema lengo la mapendekezo ya sheria ndogo kupitia katika ngazi hizo ni kuangalia kama sheria iliyotungwa haikinzani na sheria nyingine za nchi ambazo zimetungwa na Bunge au kukinzana na Katiba ya nchi.

Alisema endapo sheria hiyo itapitiwa kwenye ngazi fulani kuanzia mkoani mpaka kwa waziri na ikaonekana ina dosari, mamlaka husika inayo haki ya kuifanyia marekebisho.

Kwangula alisema kuwa wakati sheria hiyo ikirejeshwa kwenye halmashauri kutoka kwa waziri mwenye dhamana iliambatana na barua iliyowaarifu mabadiliko yaliyofanyika na sababu zake.

Kwangula aliisoma barua hiyo mbele ya madiwani na kueleza kuwa huo ni mtazamo wa ngazi za juu na kwamba baraza hilo halina mamlaka ya kuyapinga bali kuitumia sheria hiyo kama ilivyorekebishwa na waziri mwenye dhamana.

Baraza hili lilitunga sheria hiyo ambapo kifungu hicho kilisomeka 'Mtu yeyote atakayesafirisha mazao zaidi ya tani moja kutoka kata moja kwenda kata nyingine na nje ya Wilaya ya Mbarali atapaswa kulipa ushuru, lakini ilipofika kwa waziri ilipitiwa na wataalam ambao waliona kuna kasoro na wakabadilisha kifungu hicho ambacho sasa kinasomeka 'Mtu yeyote atakayesafirisha mazao zaidi ya tani moja kutoka eneo lolote la halmashauri atapaswa kulipa ushuru, nasi hatuwezi kupinga mamlaka ya juu hivyo tunapaswa kutii," alisema Kwangula.

Baada ya maelezo hayo madiwani walionekana kutoridhishwa na uamuzi wa serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kufanya marekebisho hayo bila kuwashirikisha na kutaka sheria hiyo itumike kama ilivyobadilishwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalib Lubandamo alimtaka mwanasheria wa halmashauri kutoa ufafanuzi wa kisheria ikiwa hali hiyo imejitokeza nini kifanyike.

Mwanasheria wa Halmashauri alisema kutokana na idadi kubwa ya madiwani kuondoka, baraza haliwezi kuendelea na hivyo linapaswa kuahilishwa mpaka hapo akidi ya kikao itakapotimia.

Lubandamo alisema kutokana na mkanganyiko huo, ipo haja ya wanasheria wa TAMISEMI kuja kutoa ufafanuzi ili madiwani wote wawe na uelewa wa pamoja.



# Viongozi Wizara ya Ardhi, Utalii wateta kuhusu utoaji vibali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale wamekutana kujadili uharakishaji wa utoaji wa vibali vya ujenzi hasa kwa maeneo yanayogusa sekta ya utalii Zanzibar.

Lengo la kikao hicho ni kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazozikabili wizara hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kikao hicho Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema kumejitokeza changamoto ya ucheleweshaji wa kupata vibali kwa ajili ya ujenzi wa miradi inayohusiana na sekta ya utalii.

Dk. Mngereza alisema wizara zote zimekubaliana kuharakishwa kwa upatikanaji wa vibali hivyo, kwa kuigaza Mamlaka ya Udhibiti na Uendelezaji wa Mipango Miji na Vijiji (DCU) kushirikiana na Wizara ya Utalii ili kutoa vibali kwa haraka.

Dk. Mngereza alisema katika kupatia ufumbuzi changamoto hiyo, Wizara ya Ardhi tayari imekamilisha mfumo wa utoaji wa vibali vya ujenzi ambao utanza kazi karibuni ambapo kupitia mfumo huo haitomlazimu mwananchi kufika katika taasisi kupata huduma, badala yake ataweza kuomba kibali kwa kutumia mfumo uliondaliwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Fatma Abdulla Khamis alisema uongozi wa Wizara ya Utalii umeona ipo haja ya kukaa pamoja ili kuzipatia changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya utalii.

Alisema sekta ya utalii ni sekta mtambuka ambayo imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi ambapo hivi hoteli zipatazo tano za kitalii ziliungua moto jambo lililosababisha kushindwa kutolewa kwa huduma ya dharura kulikosababishwa na ujenzi holela usiozingatia mipango miji.

Aidha, alisema kumejitokeza tabia kwa baadhi ya wageni kununua maeneo bila ya kufuata utaratibu na kujenga nyumba kwa ajili ya makazi na biashara jambo ambalo halikubali kisheria na taratibu za nchi.

Katika kulipatia ufumbuzi suala hilo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Fatma Abdullah Khamis alisema kupitia kikao kazi hicho kutakuwa na mwendelezo wa vikao kwa kuandaa utaratibu maalumu utakaotoa mwongozo juu ya makazi kwa wenyeji na wageni.

Kadhalika alitoa wito kwa baadhi ya wananchi pamoja na wanasheria kufuata utaratibu wakati wanaposhirikiana na wageni katika suala la uuzaji na ununuzi wa ardhi ili kupata wawekezaji wenye tija.

# Mataifa 40 kushiriki mkutano masuala ya moyo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NCHI zaidi ya 40 zinatarajia kushiriki mkutano wa kimataifa unaohusiana na masuala ya moyo, utakaofanyika leo visiwani Zanzibar.

Mkutano huo unatarajiwa kufunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango ambao utakuwa na washiriki zaidi ya 500.

Mkutano huo ambao umeandaliwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ambao utawashirikisha wataalam wa magonjwa ya moyo kutoka nchi mbalimbali za Afrika na Ulaya ambao utafungwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi kesho.

Akizungumza na waandishi wa habari jana visiwani Zanzibar, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Peter Kisenge, alisema serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa taasisi hiyo kwa vifaa na rasilimali watu.

Alisema taasisi hiyo sasa imekuwa ni kimbilio la wagonjwa kutoka nchi mbalimbali kupata huduma, hivyo mkutano huo unaofanyika visiwani Zanzibar utawawezesha madaktari kubadilishana uzoefu na madaktari bingwa wanaotoka nchi mbalimbali.

Mkurugenzi huyo alisema kumekuwa na mafanikio makubwa ya teknolojia katika matibabu ya moyo, hivyo mkutano huo watalamu watajifunza katika kutumia teknolojia hiyo katika kumhudumia mgonjwa wa moyo.

Aidha alisema kuna ongezeko la wagonjwa wengi wa maradhi ya moyo na asilimia 95 ambayo ya wagonjwa wakipelekwa nje ya nchi kupata matibabu, hivi sasa wanapatiwa matibabu katika taasisi ya JKCI.

uniani hupoteza maisha kutokana na magonjwa ya moyo na takwimu zinaongezesja kwa sababu ya hali ya maisha uliotokana na unywaji wa pombe uliokithiri, uvutaji wa sigara, unene wa kupundukia na watu kutofanya mazoezi.

Mtaalamu huyo alisema rika la wanaoathirika na ugonjwa huo ni kutoka miaka 40 hadi 50 lakini wapo watoto ambao wamepata tatizo hilo tangu walivyozaliwa, hivyo ni vyema kutoa elimu kwa jamii katika kujikinga na ugonjwa huo.

Kaimu Mwenyekiti Bodi ya Wadhamini ya JKCI, Asha Ressa, alisema mkutano huo utaangalia maendeleo hasa ikizingatiwa teknolojia mbalimbali zinatumika, hivyo ni vyema kuwa na watu wenye uwezo wa kutumia teknolojia hiyo katika kutoa huduma bora.

"Tunatamani nchi zetu za Afrika kutoa huduma mbalimbali za matibabu ili watu kupata huduma nzuri kwa gharama ambayo kila mlengwa kumudu kulipia" alisema.

Miongoni mwa nchi ambazo zitashiriki mkutano huo ni Misri, Uturuki, China, Uingereza, Israei, India, Marekani, Zambia, Rwanda, DRC, Kenya, Uganda, Burundi na Tanzania.



Meneja wa Kukabiliana na maafa wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Samwel Katamba (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, Mikocheni, Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio ya chama hicho ya kukabiliana na maafa yaliyotokea katika mikoa mbalimbali hivi karibuni. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano, Seki Kasuga na mmoja wa wafanyakazi wa kujitolea wa chama hicho, Erick Anthony. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wananchi waonywa matumizi dawa za asili kutibu macho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kuacha kutumia dawa za kienyeji katika kutibu ugonjwa wa macho 'red eyes' ambapo dawa hizo zimeanza kuleta madhara kwa wagonjwa ikiwemo kupata upofu.

Hayo yalisemwa juzi visiwani hapa na Mratibu wa Afya ya Msingi ya matibabu ya macho kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Rajab Mohammed wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya ugonjwa huo pamoja na madhara yake.

Alisema bado jamii inahamasisha kutumia tiba ambayo siyo sahihi katika kutibu ugonjwa huo ikiwemo mkojo, maji ya dafu, maji chumvi, mafuta ya taa na majani ya dawa asili ikiwemo kivumbasi, hali ambayo imeshaleta athari na wagonjwa saba ambao wameshapofuka macho.

"Jumla ya wagonjwa saba wamelazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja baada ya kutumia dawa zisizo sahihi na kupata upofu akiwemo mtoto mwenye umri wa miaka 11," alisema.

Alisema watu 12,860 wameripotiwa kuugua ugonjwa huo ambao wamefika katika vituo vya afya na hospitali Unguja na Pemba.

Aidha alisema hivi sasa wimbi la wagonjwa wa macho mekundu limeanza kupungua kutokana na kazi kubwa inayofanywa na serikali kwa kushirikiana na waandishi wa habari katika kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Katika hatua nyingine, akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi za CCM Kisiwandui Katibu wa NEC, Idara ya Itikadi, Mafunzo na Uenezi wa chama hicho, Khamis Mbeto Khamis alisema chama kinawajibu wa kuwalinda wananchi wake kwa kuwapa elimu juu ya ugoniwa huo wa macho.

Hivyo aliwataka wananchi kuacha kutumia vitu ambavyo havijashauriwa na daktari ambavyo tayari baadhi ya watu vimeshawaletea athari ikiwemo kupoteza uoni.

Alisema macho ni kiungo muhimu katika uhai wa binaadamu na CCM imeona isikae na kuwataka wananchi kufuata maelekezo wanayopewa na daktari.

Alisema miongoni mwa maelekezo ya wataalamu wa afya ni kunawa mikono mara kwa mara, kuacha kupeana mikono na mtu anapohisi dadilili za ugonjwa huo kufika haraka katika kituo cha afya ili kupata matibabu sahihi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/ KINONDONI**
**SHAURI LA COMMERCIAL NO. 25549 YA 2023**
**BANK OF AFRICA (T) LTD..........................MDAI**
**VERSUS**
**MUSA LUCHACHE LUGWIGWA............MDAIWA**

**KWA: MUSA LUCHACHE LUGWIGWA**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya Wilaya binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 15th Mwezi Februay Mwaka 2024 saa mbili (2:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 31st Mwezi January Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KINONDONI/KIVUKONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/ KINONDONI**
**SHAURI LA COMMERCIAL NO. 25551 YA 2023**
**BANK OF AFRICA (T) LTD..........................MDAI**
**VERSUS**
**ANSILA DAGOBERT KOMBA............MDAIWA**

**KWA: ANSILA DAGOBERT KOMBA**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya Wilaya binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 15th Mwezi Februay Mwaka 2024 saa mbili (2:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 31st Mwezi January Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KINONDONI/KIVUKONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/ KINONDONI**
**SHAURI LA COMMERCIAL NO. 25557 YA 2023**
**BANK OF AFRICA (T) LTD..........................MDAI**
**VERSUS**
**ANTONY SIDNEY MKOLOMO............MDAIWA**

**KWA: ANTONY SIDNEY MKOLOMO**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya Wilaya binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 15th Mwezi Februay Mwaka 2024 saa mbili (2:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 31st Mwezi January Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KINONDONI/KIVUKONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/ KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NO. 25554 YA 2023**
**BANK OF AFRICA (T) LTD..........................MDAI**
**VERSUS**
**LYDIA PETER KAMWAGA............MDAIWA**

**KWA: LYDIA PETER KAMWAGA**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya Wilaya binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 28 Mwezi 02 Mwaka 2024 saa mbili (2:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 31st Mwezi 01 Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KINONDONI/KIVUKONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NO. 87 YA MWAKA 2023**
**JAMES FRANCIS MBATIA...............MDAI**
**DHIDI YA**
**JOSEPH ROMAN SELASINI.............MDAIWA**

**KWA: JOSEPH ROMAN SELASINI – POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo ya madai yameelezwa katika nakala ya madai ambayo yanaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 21/02/2024 saa 9:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa A.M. LYAMUYA – HAKIMU MKAZI MKUU kwa ajili ya 1st PTC.

**ANGALIA:**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 31 Mwezi JANUARI, 2024.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**FORM II**
**SMM 1994 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Mwambao Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Ombi la ndugu **RAMADHANI ABDU KAWAMBWA** kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi namba 17/2024 ya Marehemu **TABU KONDO PANGARA.** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi hii wakitaka mnamo tarehe 29/02/2024 kabla huyu mwombaji hatateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hii.

Wasia wa Marehemu **HAUPO.**

MAHAKAMA YA MWANZO MWAMBAO - BAGAMOYO
TAREHE: 07/02/2024

---

**IN THE DISTRICT COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1025 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PASTORY MTABINGWA FAIKO DECEASED OF BUKOBA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY RAYMOND PASTORY FAIKO ............PETITIONER**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above- named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 23th day of February 2024.

The Will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court.

Dated at Bukoba this 2nd day of February 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE BUKOBA DISTRICT COURT.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**SHAURI LA ARDHI NA. 13 YA 2022**

- **HAMISI SAIDI ALLY (As administrator of estate of late SAIIDI ALLY SUFIANI)**
- **ABDALLAH SAIDI ALLY (As administrator of estate of late SAIDI ALLY SUFIANI)........WADAI**

**DHIDI YA**

- **THE CITY COUNCIL OF DODOMA** • **EDISON M. TIBAIJUKA**
- **INNOCENT MALLYA** • **MALCELINA ANTHONY MUNISH**
- **RUTA JAMES KAKOKI** • **ASIMWE LOVINCE RWIGUZA**
- **ESTANSIA ASANTERABI SHOO** • **NELSON SYDNEY MAWALA**
- **GODFREY RENATUS NYONI** • **PHILBERT PHILMON LUTALA**
- **CHRIATINA MICHAEL MZUKA** • **THE ATTORNEY GENERAL...... WADAIWA**

**KWA**
**1.MALCELINA ANTONY MUNISH, 2. RUTA JAMES KAKOKI, 3.ASIMWE LOVINCE RWIGUZA, 4.GODFREY RENATUS NYONI, 5. PHILBERT PHILMON LUTALA,**
**6. CHRIATINA MICHAEL MZUKA**

**POPOTE PALE WALIPO**
**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI NA.13 YA 2022 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**

**MNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya MHE. A.J MAMBI, JAJI wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma , saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Jumatano tarehe 14/2/2024.

**HIVYO;** Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .

**NA ENDAPO;** Hamtafika nyinyi au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakanyoamua pasipo nyinyi au wakili wenu kuwepo.

**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 18/10/2023.

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**YONAH DAUD SHILINGI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1223/0075/2016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIMALI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/18231/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI ARUSHA**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 87/02 YA 2023**
**ANNEY ANNEY...............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**TEONAS MCHANA............1 MJIBU MAOMBI**
**SAILESHI GORDAN LAXMAN T/A**
**SAIBABA EXPRESS............2 MJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**TEONAS MCHANA**
**POPOTE MLIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Arusha tarehe 20/02/2024 saa tatu kamili asubuhi (9:00)

Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe wenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi haya yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 16/1/2024

J. E. FOVO
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**
**SHAURI DOGO NAMBA 322 LA 2023**
**MHANGA PEZE MBEGA............. MDAI**
**DHIDI YA**
**UMOJA MANG'OMBE NA WENZAKE WANNE........WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: JOHN BETRI MATELEMKI, MASHIMI BETRI MATELEMKI, SHIMOLI BETRI MATELEMKI, JUMA BETRI MATELEMKI**

MNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMEFUNGUA SHAURI DHIDI YENU KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MKOA WA MWANZA, OMBI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 07/03/2024 KATIKA CHUMBA CHA BARAZA, JENGO LIKO MKABALA NA MAHAKAMA MWANZO MWANZA MJINI BARABARA YA MAKONGORO.

KWA HIVYO MNATAKIWA KUHUDHURIA KATIKA BARAZA SIKU HIYO NYIE MWENYEWE , WAKILI WENU AU MTU MWINGINE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUJIBU OMBI HILO.

KAA- MKIJUA KUSHINDWA KUFIKA BARAZA LITASIKILIZA OMBI HILO NA KUTOA UAMUZI BILA NINYI KUWEPO.

IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA BARAZA LEO TAREHE 07/02/2024.

**PAULOS S. LEKAMOI**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MWANZA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA KWIMBA**
**KITUO CHA NGUDU – MJINI**
**MWANZA**
**SHAURI LA MADAI/NDOA NAMBA 04/2024**
**SAMWEL LEONARD NZUAMKENDE.............MDAI**
**DHIDI YA**
**NEEMA GOODLUCK KANZA.............MDAIWA**

**MADAI YA TALAKA NA MATUNZO YA MTOTO**

**KWA: NEEMA GOODLUCK KANZA**
**NGUMO "B"**
**0753514201**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMEFUNGUA SHAURI DHIDI YAKO KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA KWIMBA KWA MADAI YA TALAKA NA MATUNZO YA MTOTO.

UNAAMRIWA NA MAHAKAMA HII: UHUDHURIE MBELE YA MAHAKAMA HII TAREHE 27/02/2024 SAA 02:00 ASUBUHI BILA KUKOSA KATIKA SHAURI LILILOTAJWA HAPO JUU NA NILAZIMA KULETA HATI ZOTE ZINAZOHUSU SHAURI HILO KWA AJILI YA KUJITETEA KATIKA SHAURI HILO.

ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA, NA MAAMUZI KUTOLEWA.

IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA MAHAKAMA LEO TAREHE 06/02/2024

**HAKIMU WA MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**MJINI - NGUDU**

---

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: advertise@guardian.co.tz**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji wa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MCHANGANYIKO

# Benki Kuu Nigeria yafichua madudu

**ABUJA, Nigeria**

BENKI kuu ya Nigeria imesema imegundua fedha za kigeni zenye thamani ya dola bilioni 2.4 zaidi ya Sh. Trilioni sita ambazo zinaitishwa kwa njia ya udanganyifu, kutokana na uchunguzi wa dola bilioni saba (Sh. Trilioni 17.7) zilizokuwa zikisubiri kukabidhiwa wenyewe.

Benki hiyo ilisema kwamba ufichuzi huo utapunguza changamoto zilizosababishwa na uhaba wa fedha za kigeni nchini humo, ikidai kuwa madai kwa njia ya udanganyifu huenda yakaathiri uchumi wa Nigeria.

Ilielezwa kuwa ugunduzi huo ni kutokana na uchunguzi wa kina uliofanywa na kampuni ya kimataifa ya kifedha ya Deloitte kwa niaba ya Benki Kuu ya Nigeria.

Benki hiyo ilisema kwamba ufichuzi huo ni wa kutisha, wakati kukiwa na stakabadhi bandia, watu wasiokuwepo na wanaodai fedha za kigeni, na wakati mwingine watu ambao wamepokea fedha za kigeni bila kutoa maombi rasmi, ikielezwa kuwa baadhi ya watu pia walipokea fedha za kigeni walizodai katika benki hiyo.

Gavana wa benki hiyo Olayemi Cardoso, alisema kwamba hawatatoa fedha kwa maombi yasio halali, wakati mchambuzi wa masuala ya kiuchumi, jambo lililosifiwa kama hatua nzuri ya kulinda uchumi.

"Tunapiga hatua zinazofaa, ikizingatiwa kuwa sasa tayari tumeshughulikia takriban asilimia 50 ya maombi, ikibaki asilimia sawa na hiyo, hilo litakapokamilika, tutaweza kuimarisha viwango vya fedha zetu. Nafikiri ni vyema kuwajibisha kila atakayepatikana akiwa na nia ya kuibia benki kuu," alisema.

Pia ilielezwa kuwa hiyo ni mara ya kwanza ndani ya miaka saba kwa hesabu za benki kuu kutolewa hadharani, na kwamba nchi hiyo imekuwa ikikabiliwa na uhaba mkubwa wa fedha za kigeni, suala ambalo limedumaza ukuaji wa kiuchumi, kushuka kwa thamani ya naira, pamoja na mfumuko wa bei za bidhaa.

Taarifa ya benki hiyo ilibainisha kwamba hadi sasa Nigeria imelipa takriban dola bilioni 2.3 (Sh. Trilioni 5.8) zinazoitishwa, zikiwemo zile zinazodaiwa na mashirika ya ndege pamoja na sekta za viwanda na nishati.

Mwanauchumi na mratibu wa Kituo cha Haki za Kijamii Justice Onyekprere, alisema kwamba ufichuaji uliofanywa hautasaidia kufufua uchumi wa Nigeria.

"Kuna madeni mengine yaliopo, hilo halitatatua lolote, kiwango cha sarafu kwa upande wa thamani kimezidi sera za fedha za benki kuu. Inahusiana zaidi na suala la uongozi, kwenye makadirio, viwanda, elimu na sera za afya.

"Ulisikia gavana wa benki kuu akieleza bunge kwamba utalii wa afya pamoja na ulipaji wake wa ada ulitumia takriban dola bilioni 40 (Sh. Trilioni 101.3) ndani ya miaka 10, hiyo ni sawa na takriban dola bilioni nne zaidi ya Sh. Trilioni 10 kila mwaka," alisema.

Hata hivyo Onyekpere alisema kwamba ufichuzi huo unaashiria matatizo zaidi kwenye mfumo wa fedha za kigeni wa Nigeria, ambayo yanahitaji kushughulikiwa.

**VOA**

# Daktari jela kupokea rushwa ya Sh. 70,000

**Na Mwandishi Wetu, LINDI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Lindi, imemhukumu Daktari wa Hospitali ya Mkoa wa Lindi (Sokoine), Dk. Issaya Makaya (37) kifungo cha mwaka mmoja gerezani kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 70,000 kutoka kwa mgonjwa aliyefika hospitalini huko kupata matibabu.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Maria Batraine baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliowasilishwa mahakamani, pia mshtakiwa kukiri kosa lililokuwa linamkabili.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Hakimu Batraine alimpa mshtakiwa nafasi ya kujitetea, naye akaomba mahakama isimpe adhabu kali kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza, anayo familia inayomtegemea akiwamo mke na watoto wawili, hivyo akipewa adhabu kali watakosa huduma yake.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batraine alimwuliza mwanasheria wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Fatma Chimbyangu kama anazo kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa, naye akadai hana, huku akiiomba mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwa na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

"Mheshimiwa sina kumbumbu zake, hivyo ninaiomba mahakama yako tukufu kumpa adhabu kulingana na kosa lake, ikizingatiwa yeye ni mtumishi anayelipwa mshahara na serikali kwa kazi ya kuhudumia jamii," alidai Chimbyangu. Hakimu Batraine, akitoa hukumu katika kesi hiyo Na. 03 ya mwaka 2024, alisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili na kumhukumu daktari huyo kulipa faini ya Sh. milioni moja, akishindwa akatumikie kifungo cha mwaka mmoja gerezani. Mshtakiwa alilipa faini.

Awali ilidaiwa mahakamani huko na mwendesha mashtaka wa TAKUKURU Mkoa wa Lindi, Chimbyangu, kwamba Dk. Lucas alikamatwa Februari 6 mwaka huu saa sita mchana ndani ya jengo la Hospitali ya Sokoine, mjini Lindi akipokea Sh. 70,000 aliyoomba kutoka kwa mgonjwa aliyelazwa akisubiri kufanyiwa upasuaji.

Mwanasheria huyo alidai mgonjwa huyo alikuwa amekamilisha taratibu zote ikiwamo kulipa gharama zote za matibabu na kitanda, lakini mshtakiwa aliendelea kumtaka ampe kiasi hicho cha fedha kama bahashishi yake, ndipo ndugu aliyemsindikiza mgonjwa alipotoa taarifa na mtego ukaandaliwa na kumtia nguvuni.



Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambalo limefanikiwa kuzima jaribio ya waasi wa M23 walipotaka kuutwaa mji wa Sake, jana. **PICHA: MTANDAO.**

# TCRA yaonya watumiaji mitandao kuhusu uhalifu

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeonya watumiaji huduma za mawasiliano dhidi ya uhalifu wa mtandaoni.

Ofisa Mwandamizi Mkuu wa Mawasiliano TCRA, Semu Mwakyanjala, alisema jana kuwa kuna haja kila mtumiaji huduma za mawasiliano kwenye mtandao wa intaneti kufuata sheria na taratibu zinazosimamia matumizi ya mitandao ya kijamii na huduma za intaneti.

"Ni muhimu tukumbushane kwamba ipo Sheria ya Makosa Mtandaoni ya Mwaka 2015 ambayo imeweka bayana makatazo kadha wa kadha, ikiwamo zuio la kuchapisha chochote kuhusu watu wengine bila ridhaa yao," alisisitiza na kuongeza kuwa kuchapisha taarifa za upotoshaji kwenye mtandao ni kosa kwa mujibu wa sheria hiyo.

"Mtu atakayechapisha taarifa au data katika picha, maandishi, alama au katika namna nyingine yoyote katika mfumo wa kompyuta, akijua kwamba taarifa au data ni za uongo na zinaudanganya umma, atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Sh. milioni tano au kutumikia kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja," alisisitiza.

Alikumbusha pia umuhimu wa kusambaza taarifa zenye uhakika na zinazotolewa na vyanzo rasmi vya habari, ili kuzuia usambazaji taarifa hatarishi zikiwamo zinazoipotosha jamii, picha au video za utupu, vurugu au vitisho, akionya kuwa vitendo hivyo ni kosa chini ya Sheria ya Makosa ya Mtandaoni.

Kuhusu kutumia jina la mtu mwingine mtandaoni, alisema ni kinyume cha sheria na kitendo cha mtumiaji huduma za mtandaoni kutumia utambulisho usio wake, kunaweza kusababisha adhabu, ikiwa ni pamoja na faini au kifungo kulingana na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya 2015.

Alisema baadhi ya watumiaji wa mitandao wamekuwa na kawaida ya kujivika uhusika usiokuwa wao wakitumia majina ya viongozi na watu mashuhuri ili kujipatia mali zikiwamo fedha isivyo halali na kwamba matendo hayo ni jinai, akiwaasa watumiaji wazingatie kutumia utambulisho halisi badala ya kutumia majina au taswira za watu wengine.

Kuhusu kuingilia mifumo ya kompyuta bila ridhaa, alionya kuwa sheria inakataza kitendo hicho, maarufu kama hacking, na atakayepatikana na hatia atawajibika kutozwa faini au kutumikia kifungo.

Mwakyanjala pia alisisitiza kuwa kuchapisha au kutoa ponografia za watoto kupitia mfumo wa kompyuta ni kosa kwa mujibu wa sheria na kuongeza kuwa TCRA imewasilisha ujumbe huo ukiwa ni mwendelezo wa kampeni za mamlaka hiyo kuwaelimisha wananchi na watumiaji huduma mbalimbali za mawasiliano zikiwamo za mtandao wa intaneti.

"TCRA inatoa wito kwa watumiaji wote wa mtandao kufuata sheria na taratibu, ili kuhakikisha wanajilinda na kuepuka adhabu zinazoweza kutokea kutokana na vitendo vya uhalifu mtandaoni," alisisitiza.

# TIMU 3 ZAONYESHA UGUMU NYUMBANI CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za KenGold, TMA FC na Mbeya Kwanza hazijapoteza mechi yoyote zikicheza nyumbani na kuonyesha ugumu katika Ligi ya Championship inayoendelea nchini.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) pamoja na za dawati michezo la Nipashe, zinaonyesha kuwa timu hizo tatu ni ngumu mno kufungika zikicheza kwenye viwanja vyao vya nyumbani.

KenGold inatumia Uwanja wa Sokoine Mbeya, TMA inacheza mechi zake Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha wakati Mbeya Kwanza inautumia Uwanja wa Nangwanda Sijaona uliopo Mtwara kama uwanja wake wa nyumbani.

Timu za KenGold na TMA zimecheza mechi 10 nyumbani bila kupoteza, wakati Mbeya Kwanza imecheza mechi nane bila kupoteza.

**KenGold pia ndiyo timu ili yozoa pointi nyingi ikicheza ugenini, ikipata pointi 22 katika michezo 10 iliyocheza, ikifuatiwa na Pamba FC ikiyokusanya pointi 20 katika mechi 10, Mbeya Kwanza ikipata pointi 19 kwa mich ezo 12, Biashara United pointi 18, mechi 10, TMA, pointi 18 mechi 10 na Mbuni FC imekusanya pointi 14 kwa michezo 10.**

Takwimu pia zinaonyesha kuwa Biashara United inaongoza kwa kukusanya pointi nyingi ikicheza uwanja wake wa nyumbani ambao ni, Karume, Musoma mkoani Mara.

Katika mechi zake 10 imezoa pointi 25, ikifuatiwa na timu za Pamba, Mbuni na Mbeya City, ambazo zimepata pointi 23 kila mmoja kwa mechi 10 ambazo kila timu imecheza huku KenGold ikizoa pointi 22 kwa michezo 10 iliyocheza.

Katika msimamo wa jumla, KenGold inaongoza ligi ikiwa na pointi 44, ikifuatiwa na Pamba yenye pointi 43, Biashara United ikishika nafasi ya tatu ikiwa na pointi sawa na Pamba ikitofautiana idadi ya magoli ya kufunga na kufungwa.




Octavian Laurent wa Morogoro (kulia) akipongezwa na Juvenalius Rugambwa ofisa habari wa Betika, baada ya kuibuka mshindi wa wiki hii wa promosheni ya Betika. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# *Laurent ashinda televisheni ya Twende Zetu AFCON*

**Na Mwandishi Wetu**

OCTAVIAN Laurent wa Morogoro amekuwa mshindi wa 16 kutwaa televisheni ya inchi 70 iliyotolewa na Kampuni ya kubashiriki matokeo ya mechi ya Betika pamoja na Tigo.

Laurent ambaye ni fundi simu na TV alikabidhiwa zawadi yake hiyo jana pamoja na king'amuzi cha DStv kilicholipiwa mwezi mzima pamoja na dishi alisema kuwa awali alikuwa haamini kama kweli ameshinda TV hiyo.

Alisema kuwa vijana wa mtaani kwake walikuwa wakimtania kuwa ametapeliwa na walimshawishi kutoenda Dar e Salaam kwani atapoteza nauli yake bure na wala hiyo TV hataipata.

Alisema kuwa baada ya kupata TV hiyo sasa vijana wote mtaani kwao Morogoro wataamini na kuwa tayari kucheza shindano lolote la Betika ili kupata zawadi mbalimbali.

Awali, akizungumza kabla ya kumkabidhi zawadi hiyo Ofisa Habari wa Betika-Tanzania, Rugambwa Juvenalius alisema kuwa Laurent ndiye mshindi wa 16 na wa mwisho kupata TV na aliwataka watu kuendelea kuchangamkia droo za Betika ili kupata zawadi mbalimbali.

Mbali na kutoa TV za inchi 70, Betika pia ilipeleka washindi sita waliokwenda Ivory Coast kushuhudia mechi za Kombe la Mataifa ya Afrika zinazofanyika nchini humo kuanzia Januari 13 hadi Februari 11.

Washindi hao walilipiwa kila kitu, ikiwemo nauli ya ndege kwenda na kurudi, malazi katika hoteli ya nyota tano, usafiri wa ndani nchini Ivory Coast pamoja na kiingilio cha uwanjani katika eneo la VIP.

Aidha, Juvenalius alisema kuwa washindi wa TWENZETU IVORY COAST KIVIP ambao walikwenda kushangilia timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, iliyoshiriki mashindano ya 34 ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2023) nchini humo wamerudi.

# Taifa ufukweni waingia kambini

**Na Saada Akida**

TIMU ya taifa ya soka la ufukweni 'Beach Stars' inatarajia kuingia kambini wiki ijayo kujiandaa na michuano COSAFA inayotarajiwa kuanza Marchi 17-25 mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa alisema wachezaji wote hata wale ambao wapo nje ya Dar es Salaam wote wataingia kambini siku ya Jumatatu.

Alisema katika uchaguzi wa kikosi pia wataenda visiwania Zanzibar kwenye mashindano ya Beach Soccer Festival kwa kucheza mechi ya kirafiki pamoja na kuchagua wachezaji watakaoongeza nguvu kwenye timu.

"Haya mashindano ya COSAFA ni kwa ajili ya kujiandaa na Mchezo wa kukata tiketi ya kufuzu kushiriki Fainali za Afrika kwa soka la ufukweni (BAFCON), tukifanikiwa hapo tunaenda kushiriki michuano ya kombe la Dunia, itakayofanyika mwaka 2025 kwenye Visiwa vya Shelisheli," alisema Pawasa.

Fainali hizo za 13 za FIFA kwa Soka la Ufukweni zitafanyika katika bustani ya Victoria ambayo ipo kwenye Kisiwa cha Mahé nchini humo huku kikiwa kimezungukwa na maji safi na miamba ya matumbawe.

Utoaji wa haki wa kuandaa fainali hizo kwa Shelisheli ulifanywa rasmi na FIFA Oktoba 4 mwaka jana .

Kwa taifa mwenyeji, hii itakuwa ni mara yao ya pili kuandaa mashindano ya kimataifa ya soka ya Ufukweni baada ya kuandaa Kombe la Mataifa ya Afrika la Soka la Ufukweni la CAF mwaka 2015, ambalo lilishuhudia Madagascar wakitawazwa mabingwa.

# Wahindi kutoa mafunzo ya kabadi Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKUFUNZI wa mchezo wa Kabadi kutoka Nchini India wanatarajia kuendesha Mafunzo ya siku tano kwa Walimu wa mchezo huo Visiwani hapa.

Mafunzo hayo yanaanza kufanyika leo mpaka Februari 13 yakishirikisha walimu wa Vilabu saba vya Kabadi hapa Zanzibar pamoja na wadau wa mchezo huo ambao wanahitaji kujifunza kutoka katika Wilaya na Mikoa ya Unguja.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Katibu wa Shirikisho la mchezo wa Kabadi Zanzibar, Ramadhani Mrisho alisema lengo kuu la Mafunzo hayo ni kupanua wigo kwa mchezo huo Kwa kupata walimu wengi Wanawake na Wanaume.

Alisema mchezo huo kwa Visiwani Zanzibar umeanza kutambulika mpaka kufikia idadi ya timu saba za Kabadi hivyo lazima wapatikane walimu wengi ambao wataanzisha Vilabu vyao kwa ngazi tofauti.

Alisema lengo la Shirikisho hilo ni kuona ndani ya miaka miwili ijayo wanaanzisha Ligi ya mchezo huo kuanzia ngazi ya za Mawilaya pamoja na Mikoa tofauti na mwaka sasa hivi ambapo kuna Ligi moja tu.

"Tumeanza na Mafunzo haya ya walimu wa mchezo huu wa Kabadi ambao asili yake ni nchini India, yatafanyika mafunzo mengi ili kuutangaza na kuupanua mchezo huu, tunataka uchezwe katika ngazi zote"alisema Mrisho.

Mafunzo hayo yanafanyika katika ukumbi wa Baraza la Michezo Zanzibar.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE MSHAHARA MKUBWA

KYLIAN Mbappe ana mahitaji matatu ya kifedha kwa klabu yoyote inayotarajia kumsajili iwapo ataamua kuondoka Paris St-Germain msimu wa joto, ikiwa ni pamoja na mshahara wa euro milioni 50 kwa mwaka. (***Cadena Ser***)

### KELLY ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inataka kumsajili mshambuliaji wa England, Chloe Kelly kutoka Manchester City na kumfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kuwa mchezaji anayelipwa zaidi kwa wanawake barani Ulaya. (***Mail***)

### TONEY ANUKIA MAN

MANCHESTER United ipo katika nafasi nzuri zaidi kuliko Arsenal kupata dili la kumnunua mshambuliaji wa Brentford ya England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, ambaye thamani yake ni pauni milioni 80, huku Chelsea wakitarajiwa kuangazia zaidi mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25. (***TeamTalks***)

### FERNANDEZ HAONDOKI

WAKALA wa kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 hana nia ya kuondoka Chelsea baada ya mashaka kuibuka kuhusu mustakabali wake katika klabu hiyo ya Stamford Bridge. (***AS***)

### LINGARD ATUA FC SEOUL

KIUNGO mshambuliaji wa zamani wa Manchester United na England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 31 amekubali mkataba wa miaka miwili na FC Seoul, pamoja na chaguo la mwaka zaidi. (***Sky Sports News)***

### ERIKSEN HATANUNULIWA

KLABU ya Galatasaray haitamnunua kiungo wa kati wa Manchester United na Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 31, kabla ya soko la uhamisho la Uturuki kufungwa wiki hii, lakini wananuia kutoa ofa msimu wa joto. (***ESPN***)

### ROBINSON AFUATILIWA

KLABU ya Liverpool inamfuatilia mlinzi wa kushoto wa Fulham na Marekani, Antonee Robinson mwenye umri wa miaka 26, kabla ya uhamisho wa majira ya joto. (***Football Insider***)

### OSMAN ATAKIWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inakaribia kukubali dili la pauni milioni 17 kuishinda West Ham katika usajili wa winga wa Nordsjaelland, Ibrahim Osman mweye umri wa miaka 19 raia wa Ghana. (***Standard)***

### BENZEMA ASUSIA MAZOEZI

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Karim Benzema mwenye umri wa miaka 36, aliondoka kwenye mazoezi ya Al-Ittihad baada ya kuagizwa kufanya mazoezi kivyake na kocha, Marcelo Gallardo. (***Marca)***

### TOMASSON KUTIMKA

KOCHA wa Blackburn Rovers, Jon Dahl Tomasson anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Championship baada ya mechi nane bila ushindi. (***The Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NIGERIA VS IVORY COAST, FAINALI YA KIBABE JUMAPILI

**ABIDJAN,** Ivory Coast

PAMBANO kubwa la soka litazikutanisha Nigeria dhidi ya Ivory Coast kwenye fainali ya michuano ya mataifa ya Afrika, AFCON, Jumapili.

Mchezo huo wa uzani wa juu utashuhudia wapinzani wawili wakubwa kutoka ukanda wa Afrika Magharibi wakitafuta kutawazwa kuwa mabingwa wapya wa Afrika.

**Jumapili hiyo ya Februari 11 itashuhudia fainali ya vi zazi vya dhahabu kwenye Uwanja wa Alassane Ouatt ara jijini Abidjan nchini Ivory Coast.**

Wapinzani hawa walipokutana mara ya mwisho katika hatua ya makundi, Nigeria waliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Hata hivyo, pamoja na ushindi huo wa Nigeria, Ivory Coast itakuwa ni timu tofauti kabisa kiuchezaji

**●●● Mchezo huo wa AFCON utashuhudia wapinzani wawili wakubwa kutoka ukanda wa Afrika Magharibi...**

ukiifananisha na ile ya hatua ya makundi.

Na Nigeria wanajua kwamba kuwazuia Tembo hao kushinda AFCON ya tatu kwenye ardhi ya nyumbani sio jambo rahisi.

Kwa kocha wa Nigeria, Jose Peseiro, kumzidi akili na maarifa bosi wa Ivory Coast, Emerse Fae litakuwa jambo muhimu zaidi kwake.

Mchezo wa mbinu wa Peseiro uliiongoza Nigeria kuiondoa Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti ya kusisimua kwenye nusu fainali ya kwanza Jumatano.

Lakini Fae pia alionesha ukubwa wake wa kuifunga DR Congo 1-0 katika nusu fainali ya pili.

Mengi yatategemea vita kati ya Peseiro na Fae kwenye kipute hicho.

Kwenye uwanja, nyota zitang'aa chini ya taa za Abidjan, huku Ivory Coast ikijivunia wachezaji nyota kama Nicolas Pepe na mshambuliaji mahiri wa Dortmund, Sebastien Haller.

Hata hivyo, Nigeria wana vipaji kama Victor Osimhen wa Napoli na William Troost-Ekong katika safu zao.

Mchezo huo kwa namna yoyote utakuwa mgumu kwa timu zote mbili.

Yeyote atakayeshinda, ndiye atakuwa bingwa mpya wa bara la Afrika.

# SERIKALI YA HONG KONG SASA YAWAJIA JUU MESSI, MIAMI

**VICTORIA,** Hong Kong

SERIKALI ya Hong Kong imetaka majibu kutoka kwa Klabu ya Inter Miami CF na Lionel Messi baada ya Muargentina huyo kucheza mechi ya kirafiki nchini Japan siku tatu tu baada ya kukosa mechi ya kirafiki nchini kwao.

Ofisi ya Utamaduni, Michezo na Utalii ya Hong Kong ilisema katika taarifa yake kwamba, kama mashabiki, imesikitishwa sana kwamba Messi hakuweza kucheza Hong Kong kutokana na kuwa majeruhi.

"Hata hivyo, siku tatu baadaye, Messi aliweza kucheza kikamilifu na kwa uhuru nchini Japan," taarifa hiyo ilisema.

"Serikali inatumaini waandaaji na timu zinaweza kutoa maelezo ya kuridhisha."

Mashabiki wengi walisikitishwa siku ya Jumapili wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 hakuingia uwanjani wakati wa mechi ya Inter Miami iliyojaa mashabiki wengi, huku wakidai majibu na kurejeshewa fedha zao.

Kocha mkuu wa Miami, Gerardo "Tata" Martino alisema Messi alionekana kutofaa kucheza mechi ya Jumapili kwenye mechi ya kirafiki ya Hong Kong baada ya kusema kabla ya mchezo huo kwamba, kuna uwezekano angecheza.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia aliingia kama mchezaji wa akiba dakika ya 60 siku ya Jumatano katika kipigo cha Miami kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Vissel Kobe ya Japan.

"Yeyote anayenijua anajua kuwa nataka kucheza kila wakati ... haswa katika michezo hii ambayo tunasafiri hadi sasa na watu wanafurahi kuona michezo yetu. Tunatumaini kuwa tunaweza kurudi na kucheza mchezo huko Hong Kong," alisema Messi kabla ya mchezo huko Japan.

Mechi hiyo iliyofanyika Hong Kong ilikusanya mashabiki 40,000, huku watazamaji wakilipa hadi karibu dola 640 (sawa na Tsh. 1,628,800) kwa tiketi moja.

Jijini Tokyo, katika Uwanja wa Taifa wa Japan tiketi 28,614 ziliuzwa.

Gazeti la Global Times linalodhibitiwa na Serikali ya China lilisema kutokuwepo kwa Messi kulizua maswali mengi juu ya tofauti ya matibabu ya Hong Kong.

"Mechi ya Hong Kong ikawa ya pekee katika mechi sita za kirafiki za Messi za kujiandaa na msimu katika safari hii ambapo hakuwepo," gazeti la Global Times lilisema katika taarifa.

"Hali imezidisha mashaka na juu ya uadilifu wa Inter Miami na Messi mwenyewe."

Baadhi ya mashabiki walisafiri kwa saa 12 kutoka Xinjiang hadi Hong Kong kumwona Messi, gazeti la Global Times liliandika, huku kukatishwa tamaa kwa Serikali na mashabiki.

Regina Ip, mshauri mkuu wa Serikali ya Hong Kong aliandika kwenye X kwamba: "Watu wa Hong Kong wanamchukia Messi na Inter Miami kwa hili."

Miami itacheza mechi yake ya mwisho ambayo ni ya saba za kujiandaa na msimu mpya Februari 15, dhidi ya klabu ya Newell's Old Boys kabla ya kuanza mchezo wa nyumbani wa msimu wa Ligi Kuu ya Marekani, MLS, dhidi ya Real Salt Lake, Februari 21.




# Wakala akanusha Fernandez kuondoka Chelsea

**LONDON,** England

KIUNGO wa kati wa Chelsea, Enzo Fernandez anatazamiwa kubakia katika klabu hiyo, wakala wa mchezaji huyo amethibitisha huku kukiwa na uvumi kwamba, anafikiria kuondoka hapo Stamford Bridge.

Fernandez alijiunga na Chelsea Januari mwaka jana kwa ada iliyokuwa rekodi ya England kwa pauni milioni 108, akihamia London Magharibi kutoka Benfica ndani ya wiki chache baada ya kushinda Kombe la Dunia la 2022 akiwa na Argentina na kusaini mkataba wa miaka nane na nusu hadi msimu wa joto wa 2031.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye aliondoka kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar na tuzo ya mchezaji bora chipukizi, amekuwa na wakati mgumu kucheza mara kwa mara na kuhalalisha ada yake kubwa ya uhamisho.

Chelsea kwa ujumla wamekuwa na matokeo yasiyoridhisha kwenye mbio za Ligi Kuu England.

Hata hivyo, wakala Uriel Perez, amekanusha kuwa kuna mipango yoyote ya kutafuta timu mpya.

"Mchezaji hana nia ya kuondoka," alisema Perez aakiiambia AS, akipinga moja kwa moja uvumi huo.

"Viongozi wa Chelsea walikuwa wazi sana na mradi huu. Ni mpango ambao ungekuwa mgumu mwanzoni kwa sababu wachezaji wapya na wachanga walikuwa wanakuja, lakini wakati vipande vya timu vinaungana vizuri, Chelsea walikuwa wanaendelea. kusonga mbele.

"Tamaa ya Enzo Fernandez ni kuwa kwenye timu na kufanikiwa. Hatukutani na klabu yoyote au kujaribu kuzungumza na klabu yoyote. Tunajua nia ya mchezaji ni nini. Ni wazi, angependa klabu iwe katika nafasi nyingine," alisema.

Ripoti ya FootballTransfers iliyopata mvuto mkubwa kwenye mitandao ya kijamii ilisema Perez atafungua mazungumzo na "klabu mbalimbali" kutafuta fursa nje ya Chelsea.

Fernandez hakuwa mchezaji mpya pekee aliyesaini mkataba mrefu isivyo kawaida baada ya kujiunga na The Blues.

Bila kutaja majina, gazeti la The Athletic limebainisha kuwa baadhi yao "wameonyesha masikitiko yao faragha" kwa kusaini mikataba mirefu.

Wachezaji 13 kwenye kikosi hicho wana mkataba hadi angalau mwaka 2030, huku Fernandez, Mykhailo Mudryk, Moises Caicedo na Nicolas Jackson wote wakiwa wamejifungana hadi mwaka 2031.

# Ada ya Roque kupandishwa

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inatazamiwa kuona ada ya uhamisho ya Vitor Roque ikipanda hadi angalau euro milioni 55, kwa mujibu wa ESPN.

Wakatalunya hao walifikia makubaliano na klabu ya Athletico Paranaense ya Brazil msimu uliopita wa joto ambao ulitarajiwa kumfanya Roque kuhamia Hispania Julai 2024 kwa sababu za kihasibu.

Lakini mtaji wa ziada uliohitajika kumsajili mchezaji huyo ulipatikana kwa wakati na kumleta Ulaya Januari.

Barca walikubali kulipa euro milioni 30 katika malipo ya uhakika kwa Roque, na euro milioni 31 zilizosalia katika nyongeza.

Ripoti ya sasa ya gazeti la Mundo Deportivo imefichua uchanganuzi wa ada na nyongeza, na kuifanya iwezekane kuwa Wakatalunya watawajibika kulipa sehemu kubwa ya ada hiyo ifikapo mwaka 2029.

Kufikia sasa, Roque ameigharimu Barca euro milioni 5 pekee, lakini klabu itahitaji kulipa euro milioni tano nyingine katika majira ya joto na tena kila baada ya miezi sita hadi kufikia jumla ya awali ya euro milioni 30.

Kwa kadiri ya nyongeza ilivyo, Roque atagharimu euro milioni tano nyingine kwa kila msimu ambao anacheza katika zaidi ya nusu ya michezo ya Barca, hadi thamani ya euro milioni 25.

Kwa kuzingatia kiwango cha uwekezaji na uwezo wake unaonekana, hiyo inaonekana kuwa imetolewa isipokuwa kitu kitaenda vibaya au kijana anaugua majeraha.

Kufikia malengo hayo ya mechi kutachukua thamani ya jumla ya uhamisho hadi euro milioni 55.

Roque tayari ameanza kuonesha thamani yake katika msimu mgumu kwa Barca, akifunga bao la ushindi katika ushindi muhimu wa hivi majuzi wa LaLiga dhidi ya Osasuna.

Kisha alikuwa na siku nyingine nzuri akifunga dhidi ya Alaves, lakini akatolewa nje kwa kadi nyekundu ndani ya dakika 13 tu tangu aingie uwanjani.



# YANGA, NMB WAZINDUA KADI ZENYE BIMA ZA MAMILIONI

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga kwa kushirikiana na Benki ya NMB wamezindua kadi maalum ya wanachama wa timu hiyo iliyopewa jina la 'NMB, Yanga World Debit MasterCard,' ambayo mwanachama atalipa Sh. milioni moja kuipata, ikiambatana na faida kadhaa ikiwamo bima, seti ya jezi na tiketi 10 za VIP katika msimu mmoja.

Hafla ya uzinduzi wa kadi hiyo ilifanyika jana katika makao makuu ya Benki ya NMB jijini Dar es Salaam, ambako benki hiyo iliwakilishwa na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, huku Rais wa Yanga, Hersi Said na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Mzambia Andre Mtine wakiwawakilisha 'Watoto wa Jangwani'.

Katika uzinduzi huo uliokwenda sambamba na kukabidhiwa kadi kwa wanachama waliolipia, Mponzi alisema kadi hiyo yenye nembo za NMB, Yanga na MasterCard, itakuwa na faida mbalimbali ikiwamo ukataji tiketi za ndege, bima za upotevu wa mizigo na uahirishwaji safari za ndege.

"Ni kadi yenye faida lukuki, kwa sababu NMB hatujawahi kuja na jambo dogo, hatupoi. Ukishakuwa na kadi hii, utasafiri nayo kote duniani na unafanyia ununuzi na miamala katika sehemu mbalimbali duniani, ikiwamo fursa ya kukaa katika sehemu za watu maalum katika viwanja vya ndege vya kimataifa.

"Pia, NMB Yanga World Debit Black Card ambayo utaipata punde tu utakapofungua akaunti, ukiitumia kukata na kulipia tiketi ya ndege, utaingia moja kwa moja katika bima ya kupotelewa mizigo ambako utalipwa hadi Dola 3,000 (Sh. milioni 7.5), na endapo mizigo itachelewa, bima itakulipa hadi Dola 300.

"Ukinunua tiketi kwa kutumia kadi hii, unapata hadi bima ya Dola 7,500 ambazo ni karibu Sh. milioni 20 ambazo utalipwa endapo safari za ndani na nje ya nchi zitaahirishwa na zaidi ya yote utakuwa sehemu ya huduma za NMB Mkononi na mikopo ukiwamo wa Mshiko Fasta usio na dhamana wala kujaza fomu," alibainisha Mponzi.

Aliongeza ya kwamba kadi hiyo itampa mwanachama wa Yanga punguzo la bei katika ununuzi wa migahawani, 'supermarket' na vituo vya mafuta kwa kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi, huku akitoa wito kwa Wana Yanga kujitokeza katika matawi yote nchini kufungua akaunti ama kulipia kadi hiyo.

Naye Hersi mbali na kuishukuru NMB kufanikisha mchakato uliozaa kadi hiyo maalum, alipongeza kwa mafanikio makubwa iliyopata benki hiyo mwaka jana, ilivuna faida kubwa inayoakisi thamani, ukubwa na ubora wa huduma zao, unaoendana na hadhi ya Yanga.

"Huu ni mwendelezo wa masuala yanayoambatana na sherehe zetu za miaka 89 ya kuzaliwa kwa Yanga utakaofikia kilele Februari 11, tuko hapa kuzindua kadi ya kiwango cha juu kabisa katika huduma za kibenki Tanzania, kadi ambayo inamtambua mtumiaji wake kama mteja wa daraja la juu.




Rais wa Yanga, Hersi Said (wa pili kushoto) na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wa pili kulia) wakizindua kadi maalum ya benki hiyo kwa klabu hiyo jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Kadi wa Benki ya NMB, Philbert Casmiir (kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Yanga, Andre Mtine. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Gamondi akomaa na Safu ya ulinzi

INATOKA UK 24

toruhusu kufungwa alafu tupiganie pointi tatu," alisema Gamondi.

Gamondi alisema ni muhimu kwa wachezaji wote kucheza kwa ushirikiano kwenye kutimiza majukumu yao ikiwa ni kuzuia kufungwa na kufunga mabao kwenye mechi zao.

Alisema wana kazi kubwa ya kufanya kwenye kila idara kuanzia ile ya ulinzi ambayo ni muhimu kuhakikisha hawafungwi na hiyo itawapa nguvu kutafufa mabao mengi ya kushinda.

"Ni rahisi kuwa na mwendo mzuri pale unakuwa na timu ambayo haifungwi lakini ikitokea mkifungwa, presha inakuwa kubwa kwenye kutafuta mabao na kupata ushindi," alisema Gamondi.

Alisema anaimani na wachezaji wake na anajua wanapambana kuhakikisha timu inafanya vizuri na kufikia malengo yao.

Yanga jana ilikuwa ikicheza mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mashujaa na kwa sasa presha imekuwa kubwa kwenye nafasi tatu za juu katika msimamo wa Ligi Kuu.

Kabla ya mchezo huo wa jana, Yanga ilikuwa ikiongoza ligi ikiwa na pointi 34 ikifuatiwa na Azam yenye pointi 31 huku Simba ambao wapo nyuma kwa mchezo mmoja inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 29.



# Tabora United yaomba radhi, yaahidi kujipoza kwa Namungo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukung'utwa mabao 4-0 na Simba, Jumanne iliyopita kwenye uwanja wao wa nyumbani, Ali Hasaan Mwinyi, Tabora, klabu ya Tabora United imewaomba radhi mashabiki wake na kuahidi kuwapoza katika mechi ya Jumapili ijayo dhidi ya Namungo itakayochezwa kwenye uwanja huo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Thabit Kandoro amesema baada ya kutofanya vyema katika mchezo uliopita, sasa akili yao wanaielekeza kwenye mechi hiyo kwa ajili ya kupata pointi tatu ili kusonga mbele na kuacha kuangalia walipojikwaa.

Hata hivyo, kwa niaba ya klabu aliwaomba radhi mashabiki wa timu hiyo kwa kipigo kikubwa hicho ilichokipata kwa mara ya kwanza kwenye uwanja wa nyumbani huku akiahidi watafanya kila njia isijirudie tena.

"Kwanza nitumie fursa hii kuwaomba radhi mashabiki wa wapenzi wa Tabora United, ni moja katika ya mechi mbaya sana kuwahi kushuhudia kama kiongozi, sapoti wanayotupa hawastahili kwa kile tulichowapa pale, hatukuonyesha kiwango kizuri naomba watusamehe, ule siyo mchezo wetu, sivyo ambavyo tulipanga tucheze, hayakuwa maelngo ya sisi kucheza vile, tumewanguasha sana," alisema kiongozi huyo.

Akiuchanbua mchezo huo jinsi ulivyokuwa alisema wachezaji wao walicheza wakiwa chini sana na kukaa nyuma zaidi wakiwaacha Simba kutawala maeneo mengi ya mchezo

"Niseme tu tulianza tukiwa chini sana na tukacheza tukiwa nyuma na ukicheza na timu kubwa ukiwa unazuia unatakiwa uwe na nidhamu ya hali ya juu, usifanye makosa, bahati mbaya sana tukawa tunafanya makosa, hatukuwa vizuri kuzuia mipira ya adhabu ndogo, mabao mawili tulifungwa ya aina hiyo," alisema Kandoro.

Hata hivyo amewataka mashabiki wa Tabora United kusahau yaliyopita na kuendelea kuisapoti timu hiyo kwenye mchezo wao wa Jumapili dhidi ya Namungo.

# Michezo
Nipashe
Ijumaa Februari 9, 2024



Wakala akanusha Fernandez kuondoka Chelsea UK. 21




Mshambuliaji wa timu ya taifa ya Ivory Coast, Sebastien Haller (kushoto) akiwania mpira na beki wa timu ya taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kwenye mchezo wa nusu fainali ya AFCON uliochezwa juzi usiku, Haller alifungia timu yake bao pekee kwenye ushindi wa 1-0 na kuisaidia kutinga hatua fainali ya michuano hiyo ambapo watakutana na Nigeria waliowafunga Afrika Kusini kwenye nusu fainali ya kwanza. **PICHA: MTANDAO.**

## Gamondi akomaa na Safu ya ulinzi

**Na Saada Akida**

WAKATI wanachama na mashabiki wa Yanga wakilia na safu yao ya ushambuliaji kuwa butu katika kupachika mabao tangu urejeo wa Ligi Kuu, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema yeye ameanza kufanyia kazi safu yake ya ulinzi na kiungo ili kuwa na mwendo bora katika kila mechi.

Gamondi ameweka wazi kuwa safu yake ya ulinzi inatakiwa kuwa makini na kuwa na utulivu wanapokuwa wanashambuliwa.

Alisema kwa sasa ligi kuu imekuwa ngumu kutokana na kila timu kuhitaji ushindi hivyo lazima wawe makinikatika kila mchezo ambapo ameweka lengo la kwanza ni kupata pointi tatu na kutoruhusu kufungwa.

"Kwa sasa hatutakiwa kuruhusu mabao golini kwetu, ndio nafahamu tumekuwa na tatizo uidogo kwenye kufunga lakini naamini ni tatizo la muda mfupi tu, katika mbio za ubingwa hapa tulipofikia tunapaswa

INAENDELEA UK 23

# Simba, Azam mechi ya kibabe

**Thomas Wandiba SAUT , na Adam Fungamwango**

## ●●● Benchikha akiri mchezo utakuwa mgumu, Kocha Azam aisifia Simba huku akiwakosa nyota wanne...

KOCHA wa Simba, Abdelhak Benchikha amekiri kuwa mchezo wa leo dhidi ya Azam FC utakuwa mgumu na hautabiriki kutoka na ubora wa wapinzani wao lakini amesema amewataka wachezaji wake kupambana kuhakiksha wanapata ushindi.

**Wakati Benchikha, ak isema hivyo,Kocha wa Azam FC, Bruno Ferr amesema ugumu wa mchezo huo unataokana na namna kikosi cha Simba kilivyobadilika katika siku za karibuni.**

Simba na Azam zinaumana leo kwenye uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kuanzia saa 10:00 jioni huku Simba wakiwa wenyeji wa mchezo huo.

Pigo kubwa katika mchezo huo lipo kwa kocha wa Azam FC, Ferr ambaye atawakosa nyota wake nne kutokana na kuwa majeruhi baada ya kuumia kwa nyakati tofauti.

Ferr alisema leo atawakosa Sospeter Bajana na Malickou Ndoye ambao wote wana majeraha baada ya kuumia maungio ya chini ya Mguu. Pia watawakosa Abdallah Sebo aliyefanyiwa upasuaji wa goti pamoja na Alasane Dialo aliyeumia kwenye michuano ya a Mapinduzi Cup mwezi uliopita.

"Tunahitaji maamuzi mazuri katika mchezo huu, si kwa ajiri ya Azam tu bali pia na wapinzani wetu ili tuweze kupata mshindi sahihi aliyejiandaa vizuri, mchezo hautakuwa mwepesi japo nakiri Simba imebadilika sana kwa siku za karibuni, wanacheza vizuri na wamekuwa wakipata matokeo chanya, lakini na sisi tumejiandaa pamoja na changamoto ya kuwa na majeruhi ila tupo tayari kupambana na kuwapa mashabiki burudani," alisema Kerr.

Kocha wa Simba, Benchikha, akizungumza jijini Mwanza alisema Azam ni moja ya timu nzuri kwenye ligi na wana wachezaji wenye uwezo mkubwa hivyo anatarajia upinzani mkubwa kutoka kwao.

"Wachezaji wanajua umuhimu wa kushinda mechi kubwa kama hizi, tumejiandaa na tunasubiri kuona baada ya dakika 90, kikubwa nimewapa maelekezo wachezaji kuwa tunataka pointi tatu," alisema Benchikha.

Aidha, alisema anafahamu msimu uliopita Azam walikuwa moja ya vikwazo kwao kwenye mbio za ubingwa hivyo msimu wanataka kuondoa kikwazo hicho katika mbio zao za ubingwa.

"Azam ni moja ya timu iliyoivurugia mipango Simba ya kuwa Mabingwa msimu uliopita hivyo tumejipanga vyema kuwakabili kwani tunajua wanatimu nzuri ni Mechi yetu dhidi yao haijawai kuwa rahisi " alisema Kocha huyo.

Alisema mchezo huo ni muhimu sana kupata ushindi ili kukoleza mipango yao ya kutaka kutwaa ubingwa msimu huu.

Iwapo Simba itashinda itafikisha pointi 32 na kukwea hadi nafasi ya pili ya msimamo, na kama Azam itapata ushindi itafikisha jumla ya pointi 34 na kuzidi kuifukuza Yanga ambayo kabla ya mechi ya jana dhidi ya Mashujaa FC pia ilikuwa na pointi 34.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042